**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ILIYOWASILISHWA NA MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED (MBM)

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2022**

**YALIYOMO**


YALIYOMO ........................................................ i

ORODHA YA VIAMBATANISHO ................................... iii

A. UTANGULIZI ........................................................ 1

B. MUUNDO WA WIZARA ............................................ 3

C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2021 – MACHI, 2022 NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. ................................ 4

C.1 PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI. ....................................... 4

C.1.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Usafirishaji. ........................................................ 5

C.1.2. Programu Ndogo ya Pili: Miundombinu ya Usafirishaji. 11

C.2. PROGRAMU YA PILI: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ........................................................ 24

C.2.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA. ........................................................ 24

C.2.2. Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Huduma za TEHAMA. ........................................................ 31

C.3. PROGRAMU YA TATU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI......35

C.3.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Utawala na Uendeshaji. ...35

C.3.2. Programu Ndogo ya Pili: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara. ........................................................ 37

C.3.3. Programu Ndogo ya Tatu: Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba. ........................................................ 40

D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2021 HADI MACHI, 2022 PAMOJA NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. ........................................................ 42

D.1. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR..........42

D.2. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR...............48

D.3. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR. ............................54
D.4. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR. ..........................................61
E. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO.................63
F. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO. ............................63
G. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. ..................................64
H. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023..................................................65
I. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023............................66
I.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI. ...................................66
I.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji. .............................................66
I.2. PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)..............................................67
I.2.1. Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA........................................................................67
I.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA. ....................................................................68
I.3.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ....................................................................68
I.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.................................................................69
I.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ...............................................................................69
J. HITIMISHO .......................................................................69
K. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023.............72

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


Kiambatanisho Namba 1A: Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Julai 2021 - Machi 2022............74

Kiambatanisho Namba 1B: Ruhusa za Njia na Usafirishaji Julai 2021- Machi 2022............74

Kiambatanisho Namba 1C: Utoaji wa Beji Kwa Madereva na Matingo wa Gari za Abiria kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022. ............................74

Kiambatanisho Namba 2: Orodha ya Kazi za Matengenezo ya Barabara zilizopangwa Kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kupitia Mfuko wa Barabara Zanzibar.....75

Kiambatanisho Namba 3: Orodha ya Barabara za Ndani zenye Urefu wa Kilomita 275.9 zinazotarajiwa Kujengwa kwa Kipindi cha Miaka Mitano..........76

Kiambatanisho Namba 4: Orodha ya Barabara za Mjini zenye Urefu wa Kilomita 103.7...79

Kiambatanisho Namba 5: Orodha ya Barabara zenye Urefu wa Kilomita 200........................82

Kiambatanisho Namba 6: Orodha ya Miradi inayotarajiwa Kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023......................83

Kiambatanisho Namba 7A: Orodha ya Taasisi zilizounganishwa na Mkonga wa Mawasiliano kwa Kipindi cha Julai, 2021 – Machi, 2022...84

Kiambatanisho Namba 7B: Taasisi zilizounganishwa na Data Centre kwa Kipindi cha Julai, 2021 – Machi, 2022 ...................86

Kiambatanisho Namba 8: Orodha ya Minara ya

| | |
|---|---|
| | Mawasiliano inayoendelea Kujengwa katika Maeneo Mbalimbali Unguja Na Pemba ................................86 |
| Kiambatanisho Namba 9A: | Wafanyakazi Waliopata Mafunzo ya Muda Mrefu kwa Kipindi cha Mwaka 2021/2022............88 |
| Kiambatanisho Namba 9B: | Wafanyakazi Waliopata Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Kipindi chaMwaka wa Fedha 2021/2022 ............................88 |
| Kiambatanisho Namba 10: | Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Zilizopatikana kwa Kila Programu kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022 ...89 |
| Kiambatanisho Namba 11: | Mapato Yaliyokusanywa kwa Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ............................90 |
| Kiambatanisho Namba 12A: | Idadi ya Ndege zilizohudumiwa kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022 ............................90 |
| Kiambatanisho Namba 12B: | Idadi ya Abiria Waliohudumiwa katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022......................91 |
| Kiambatanisho Namba 12C: | Kampuni za Ndege zilizotumia Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kwa Mwaka 2021/2022 ..............................91 |
| Kiambatanisho Namba 13A: | Huduma za Meli ......................93 |
| Kiambatanisho Namba 13B: | Huduma za Mizigo ..................93 |

## A. UTANGULIZI.

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo.

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini, kwa kuniteua na kunipa wadhifa wa kuiongoza Wizara hii. Naahidi kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kushirikiana na viongozi wezangu na watendaji wote katika kufanikisha majukumu tuliyokabidhiwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa umahiri wake mkubwa katika kuiongoza nchi yetu. Chini ya Uongozi wake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025.

   Vilevile, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza vyema Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuleta maridhiano na kuwaunganisha Wazanzibari wote na kuhakikisha amani, utulivu na mshikamano unaendelea kudumu katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** pia nachukuwa fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawashukuru viongozi wetu hawa kwa miongozo wanayotupatia katika Wizara yetu ambayo imetuwezesha kutekeleza kazi zetu za Wizara kwa ufanisi, uwazi na kujiamini zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri, hekima na busara unazozitumia katika kuliongoza Baraza letu ambalo limekuwa likifanya kazi zake kwa umahiri mkubwa kwa manufaa ya nchi yetu. Aidha, pongezi za dhati ziende kwa Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kukusaidia kuendesha shughuli za Baraza.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati chini ya uongozi makini wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla, Mwakilishi wa kuchaguliwa na Wananchi katika Jimbo la Kwahani kwa maoni, hoja, mapendekezo, ushauri na maelekezo ambayo yanaisaidia sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Kamati hii ilipata nafasi ya kutembelea Taasisi na miradi mbalimbali iliyomo ndani ya Wizara hii na kutoa ushauri na maoni yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Ushauri na maoni wanayotupatia, tunaendelea kuyafanyia kazi kwa vitendo kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara.

7. **Mheshimiwa Spika,** matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan), Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar - ZADEP (2021- 2026), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2013), Sera mbalimbali za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), ahadi pamoja na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali. Katika utekelezaji wa mipango hiyo, Wizara imezingatia vipaumbele vikuu vya Serikali ikiwemo Maandalizi ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani (Mangapwani Integrated Port) pamoja na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ikiwemo Barabara kuu, Barabara za ndani pamoja na Barabara za Mjini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha Sekta ya Usafiri wa Anga kwa kujenga Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja na Uwanja wa Ndege wa Nungwi.

## B. MUUNDO WA WIZARA

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeundwa na Idara 3 ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano pamoja na Ofisi Kuu Pemba ambayo inaratibu Shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Aidha, Wizara hii ina taasisi nane zinazojitegemea ambazo ni; Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar, Shirika la Meli Zanzibar, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar, Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Wizara inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi nilizozitaja hapo juu.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2021 – MACHI, 2022 PAMOJA NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

9. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Bajeti kwa kutumia Mfumo wa Programu (PBB). Hivyo, taarifa hii ya utekelezaji ninayoiwasilisha imezingatia Programu za Wizara ambazo tuliziwasilisha katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuidhinishwa na Baraza lako Tukufu. Vile vile, taarifa hii inajumuisha utekelezaji wa malengo mbalimbali ya Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

10. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, kwa heshima sasa naomba uniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Programu Kuu tatu (3) za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 kama ifuatavyo: -

### C.1. PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI.

11. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za usafiri zilizo salama na endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina Programu ndogo mbili (2) ambazo ni; Usimamizi wa Usafirishaji na Miundombinu ya Usafirishaji.

### C.1.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Usafirishaji.

12. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.

**MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR**

13. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji inaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia usafiri wa barabarani kwa kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka inafanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto pamoja na kutoa leseni za njia kwa vyombo hivyo (Road License), kutoa leseni kwa vyuo vya udereva na walimu wao, kutoa leseni za madereva wanafunzi (lena), kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi, kutoa ruhusa za njia na usafirishaji wa abiria na mizigo, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kutoa vibali kwa madereva wa kigeni wanaotaka kuendesha vyombo vya moto hapa Zanzibar.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi zilizofanyika katika Programu hii ndogo kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ni kama ifuatavyo:-

a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imekagua jumla ya vyombo vya moto 47,225 Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa vipo katika hali ya uzima na usalama ambayo ni sawa na asilimia 110 ya

makadirio ya vyombo 42,922 vilivyopangwa kukaguliwa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya vyombo hivyo, 41,087 vimekaguliwa Unguja na 6,138 vimekaguliwa Pemba. **Kiambatanisho namba 1A** kinahusika.

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** Jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 12,509 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 130 ya makadirio ya ruhusa 9,618 zilizopangwa kutolewa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya ruhusa hizo 11,190 zimetolewa Unguja na ruhusa 1,319 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 1B** kinahusika.

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Mamlaka imefanikiwa kutoa leseni za usafirishaji wa gari za biashara aina mbalimbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo ambapo jumla ya leseni 12,170 zimetolewa sawa na asilimia 115 ya makadirio ya leseni 10,606 zilizopangwa kutolewa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya leseni hizo, 10,796 zimetolewa Unguja na 1,374 zimetolewa Pemba.

d. **Majaribio ya Madereva,** Mamlaka imewafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 7,463 sawa na asilimia 99 ya madereva 7,596 waliokadiriwa kufanyiwa majaribio kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Ikiwa madereva 5,849 wamefanyiwa Unguja na madereva 1,614 wamefanyiwa Pemba.

e. **Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva:** Jumla ya beji 7,575 zimetolewa kwa utingo na madereva wa vyombo vya biashara vya aina mbalimbali Unguja na Pemba sawa na asilimia 82 ya makadirio ya beji 9,316 zilizopangwa kutolewa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya beji

hizo, 6,936 zimetolewa Unguja na 639 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 1C** kinahusika.

f. **Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi:** Mamlaka imetoa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa madereva wanafunzi 12,170 Unguja na Pemba sawa na asilimia 115 ya makadirio ya leseni 10,606 zilizopangwa kutolewa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya leseni hizo, 10,796 zimetolewa Unguja na 1,374 zimetolewa Pemba.

g. **Utoaji wa Vibali kwa Madereva Wageni.** Jumla ya vibali 13,470 vya ruhusa ya kuendesha vyombo vya moto kwa wageni vimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 276 ya makadirio ya vibali 4,885 vilivyopangwa kutolewa kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Kati ya vibali hivyo 13,441 vimetolewa Unguja na 29 vimetolewa Pemba.

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imefanikiwa kurasimisha biashara ya kusafirisha abiria kwa njia ya pikipiki na bajaji ambapo hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya pikipiki (Bodaboda) na bajaji 5,273 zimesajiliwa na kupewa ruhusa ya kusafirisha abiria Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha huduma za usafiri wa barabara pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana. Aidha, jumla ya madereva 1,314 wa pikipiki na bajaji wamehudhuria mafunzo ya kuendesha biashara hiyo katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia Karume na kupatiwa vyeti na beji Unguja na Pemba.

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 2,576,454,500 na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 2,483,598,302 zimekusanywa sawa na asilimia 96 ya makadirio.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,371,800,000 ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 698,230,453 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 50.9 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, mshahara ni TSH 485,815,588 na matumizi ya kawaida ni TSH 212,414,865.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imepanga kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani pamoja na kuvifanyia ukaguzi vyombo vya moto vya binafsi na Serikali. Aidha, Mamlaka imepanga kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaotumika kwa ajili ya kuomba leseni (Zanzibar Online Driving License Application Portal) ili kuenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia pamoja na kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

19. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Usimamizi wa Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka imepanga kuanza utekelezaji wa kanuni ya utoaji wa adhabu za papo kwa papo kwa makosa ya barabarani. Mfumo wa utoaji wa adhabu hizo kwa njia ya kielektroniki tayari umeshakamilika na umeshafanyiwa majaribio.

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imepangiwa kukusanya jumla ya TSH 3,899,974,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kati ya fedha hizo, TSH 3,033,500,000 zinatarajiwa kukusanywa Unguja na TSH 866,474,000

zinatarajiwa kukusanywa Pemba. Aidha, Mamlaka imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,583,600,000 ambazo ni Ruzuku kwa matumizi ya kawaida na mishahara.

**WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR**

21. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi na uuzaji wa gari za Serikali.

22. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza yafuatayo; -

a. **Matengenezo ya Magari:** Wakala imefanikiwa kuzifanyia matengenezo gari 663 Unguja na Pemba sawa na asilimia 92 ya makadirio ya vyombo 720 vilivyopangwa kufanyiwa matengenezo kwa kipindi cha Julai, 2021, hadi Machi, 2022. Kati ya gari hizo, gari 454 ni za Serikali na 209 ni gari za watu binafsi. Aidha, jumla ya gari 617 zimefanyiwa matengenezo Unguja na gari 46 zimefanyiwa matengenezo Pemba.

b. **Utoaji wa Ushauri wa Kitaalamu Juu ya Ununuzi na Uuzaji wa Vyombo vya Moto vya Serikali:** Wakala imetoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 12 juu ya ununuzi wa vyombo vya moto. Taasisi hizo ni Tume ya Mipango, Wizara ya Afya, Kamisheni ya Uvuvi Zanzibar, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara,

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, Afisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Kwa upande wa Pemba jumla ya taasisi tatu zimepatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya uuzaji wa vyombo vya moto. Taasisi hizo ni; Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

c. **Uimarishaji wa Karakana Unguja na Pemba:** Wakala inaendelea kuziimarisha Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba kwa kuzifanyia matengenezo mbalimbali ikiwemo jengo la Karakana ya Chumbuni, Karakana ya Mombasa pamoja na Karakana ya Saateni. Aidha, Wakala imeweka CCTV Camera 20 katika jengo la Karakana lililopo Chumbuni ili kuimarisha ulinzi na usalama wa vifaa katika jengo hilo. Vilevile, Wakala imefanikiwa kutengeneza *database* ya gari zote za Serikali ambayo itasaidia kutambua idadi na aina ya gari zilizopo katika taasisi pamoja na kujua taarifa za matengenezo ya gari hizo. Pia, Wakala imeanza kutumia mfumo wa zanmalipo ili kudhibiti mapato ya Serikali. Kwa upande wa Karakana ya Pemba, Wakala imenunua vifaa mbalimbali ili kuimarisha utoaji wa huduma katika Karakana hiyo. Aidha, Wakala inaendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, jumla ya wafanyakazi saba (7) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ikiwemo za ufundi na utawala na wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika kada tofauti.

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,894,300,000 ikiwa ni ruzuku kwa kazi za kawaida na Mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla

ya TSH 821,764,343 zimetumika sawa na asilimia 44.5 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 600,807,693 ni Mshahara na TSH 220,956,650 ni matumizi ya kawaida.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.**

24. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imepanga kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto 850 vya Serikali na binafsi, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya utengenezaji wa magari, kuongeza vitendea kazi pamoja na kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi yake iliyopo Chumbuni.

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imepangiwa kukusanya jumla ya TSH 100,000,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kati ya fedha hizo, TSH 75,000,000 zinatarajiwa kukusanywa Unguja na TSH 25,000,000 zinatarajiwa kukusanywa Pemba. Aidha, Wakala imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,152,800,000 ambazo ni Ruzuku kwa matumizi ya kawaida na mishahara.

**C.1.2. Programu Ndogo ya Pili: Miundombinu ya Usafirishaji.**

26. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuwepo miundombinu ya usafirishaji iliyo bora, salama na endelevu kwa Unguja na Pemba.

**WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR (ZANROADS).**

27. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ina jukumu

la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote. Kwa kipindi cha Julai 2021, hadi Machi, 2022, Wakala wa Barabara kupitia programu hii ndogo imefanikiwa kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba kwa kiwango cha lami kama ifuatavyo: -

**a. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kinduni – Kichungwani - Kitope (km 4) na Sharifumsa – Mwanyanya - Skuli ya Bububu (km 3.8) kwa Kiwango cha Lami pamoja na Ujenzi wa Madaraja.**

28. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa barabara hizi zenye urefu wa kilomita 7.8 pamoja na ujenzi wa madaraja makubwa mawili umekamilika kwa asilimia 100. Mradi huu umetekelezwa na Mkandarasi kwa Mkataba wa TSH 8,146,017,004. Mradi huu bado umo kwenye kipindi cha uangalizi (defect liability period).

**b. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kipapo Mgelema - Wambaa (km 9.3) kwa Kiwango cha Lami.**

29. **Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa na Wakala wa Barabara. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 malengo yalikuwa ni kujenga kilomita 6 kwa kiwango cha lami na kilomita 3.8 kwa kifusi cha tabaka la kwanza. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya kilomita 4 zimejengwa kwa kifusi cha tabaka la mwisho na matayarisho ya uwekaji wa lami yameanza. Aidha, jumla ya kilomita 3.8 zimeshasafishwa na kazi za ujenzi zinaendelea. Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,203,926,281 na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 1,118,000,000 zilipatikana sawa na asilimia 50.7

c. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Maeneo Huru (Free zone) Micheweni (km 2.4) kwa Kiwango cha Lami.**

30. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa tabaka la kifusi, kalvati, misingi pamoja na uwekaji wa lami. Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala wa Barabara ilipanga kukamilisha ujenzi wa barabara yote kilomita 2.4 kwa kiwango cha lami pamoja na kuweka alama za barabarani. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi 2022, jumla ya kilomita 0.9 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kazi ya uwekaji wa lami inaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 931,232,400 na hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi 2022, jumla ya TSH 482,000,000 zimetumika sawa na asilimia 51.7.

d. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Hawaii (km 2) Kiwango cha Lami.**

31. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali ya kuijenga barabara ya Hawaii kwa kiwango cha lami. Mradi unagharamiwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar. Kazi zilizofanyika hadi kufikia mwezi wa Machi 2022, ni pamoja na kukamilisha uwekaji wa lami kilomita 1.4. Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 668,485,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022, jumla ya TSH 87,040,439 zimepatikana sawa na asilimia 13 ya makadirio.

e. **Ujenzi wa Daraja la Machui**

32. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara ilipanga kulifanyia matengenezo Daraja la Machui baada ya kuvunjika katika

mwaka wa fedha uliopita. Daraja hili lilifanyiwa matengenezo ya dharura ili liweze kutumika na jumla ya TSH 30,000,000 zilitumika kwa kazi hiyo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Daraja hili lilipangiwa kutumia jumla ya TSH 130,000,000 kwa ajili ya kulijenga upya na hadi kufikia Machi 2022, hakuna fedha iliyopatikana.

**f. Ujenzi wa Daraja la Vitongoji**

**33. Mheshimiwa Spika,** Wakala ya Barabara ilipanga kulijenga upya Daraja la Vitongoji kutokana na kuchakaa daraja hilo. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ujenzi wa daraja hili ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 750,000,000 na hadi kufikia mwezi wa Machi 2022, hakuna fedha iliyopatikana.

**g. Kazi za Matengenezo ya Kawaida ya Barabara**

**34. Mheshimiwa Spika,** Kazi za matengenezo ya kawaida ya barabara zikiwemo kazi za ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa misingi ya maji, makalvati pamoja na uzibaji wa mashimo kwa barabara za lami Unguja na Pemba zimefanyika.

**35. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 3,904,600,000 ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 2,396,752,925 zimetumika sawa na asilimia 61 ya Makadirio ya bajeti. Kati fedha hizo, mshahara ni TSH 2,243,051,510 na matumizi ya kawaida ni TSH 153,701,415.
Kwa upande wa Mfuko wa Barabara Zanzibar, Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 12,862,000,000 na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 5,458,245,087 zimepatikana sawa na asilimia 42.4 ya makadirio ya bajeti

kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbalimbali Unguja na Pemba.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.**

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Barabara Zanzibar imepanga kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba zitakazogharamiwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar ikiwemo ujenzi wa barabara ya Tumbatu yenye urefu wa kilomita 9, kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kipapo – Mgelema – Wambaa yenye urefu wa kilomita 9.3 pamoja na uwekaji wa lami katika barabara ya Kijangwani – Birikau yenye urefu wa kilomita 4.2.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wakala itaendelea kuzitunza barabara mbalimbali zilizokwisha kujengwa kwa kuzifanyia usafi pamoja na kuzifanyia matengenezo Unguja na Pemba ikiwemo barabara zilizojengwa kwa lami baridi katika Mkoa wa Kusini Pemba ambazo ni Barabara ya Mtambile – Kengeja kilomita 9.4, Mtambile – Kangani kilomita 6.4, Mizingani – Wambaa kilomita 9.7, Kenya – Chambani kilomita 3.2, ChanjaMjawiri – Tundauwa kilomita 11 na Barabara ya Chanjaani – Pujini kilomita 5.
Pia, Wakala imepanga kuweka taa za kuongozea gari kwenye makutano ya barabara katika maeneo matano (5) pamoja na kujenga madaraja mbalimbali Unguja na Pemba. Orodha ya barabara ambazo zimepangwa kufanyiwa matengenezo Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 zinaonekana katika **kiambatanisho namba 2.**

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Barabara Zanzibar imepangiwa kutumia jumla ya TSH 3,903,600,000 ambazo ni Ruzuku kwa matumizi ya

kawaida na mishahara. Aidha, Wakala imepanga kutumia jumla ya TSH 20,033,644,000 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbalimbali Unguja na Pemba.

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

39. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Miundombinu ya Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya usafiri wa nchi kavu, anga na baharini pamoja na sekta ya mawasiliano. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara kupitia Programu ya Miundombinu ya Usafirishaji imesimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ifuatayo: - Ujenzi wa Barabara ya Kizimbani - Kiboje (km 7.2), Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake Chake (km 22.1), Ujenzi wa Barabara ya Fumba – Kisauni (km 12), Ujenzi wa Barabara ya Jozani – Charawe - Ukongoroni (km 23), Ujenzi wa Barabara ya Jumbi - Tunguu (km 4.8), Ujenzi wa Barabara ya Finya – Kicha (km 8.8), Ujenzi wa Barabara ya Konde - Msuka (km 4.2), Micheweni – Maziwa ng'ombe – Kiuyu (km 7.3), Mapofu – Shumba viamboni – Tumbe Bandarini (km 11) na Barabara ya Micheweni – Shumba mjini (3.5). Aidha, barabara nyengine zinazosimamiwa na kuratibiwa kupitia programu hii ndogo ni ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kwautao (km 6.5), Ujenzi wa Barabara ya Bumbwini Skuli – Kiongwe (km 4.3), Mwera – Masingini – Bububu Kijichi (km 8), Mahonda – Pangatupu – Bumbwini (km 8), Mwera Polisi – Fuoni (km 6.1), Kama Msikitini – Kama KMKM (km 3) na Darajabovu – Miembe saba (km 3.3), Upembuzi Yakinifu wa Daraja la Uzi Ng'ambwa (km 2.2) pamoja na Ujenzi wa kilomita (km 30.5) za Misingi ya kuondoshea maji katika barabara.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Usafiri wa Anga, Idara inaendelea kusimamia na kuratibu mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi. Pia, Idara inasimamia na kuratibu Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani katika Sekta ya Usafiri wa Baharini.

41. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi zaidi, Serikali ilitoa maelekezo ya kuwa na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hivyo, Wizara kufuatia maelekezo ya Serikali, imezigawanya barabara hizo katika makundi makuu manne ambayo ni mradi wa ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa kilomita 125.1, mradi wa ujenzi wa barabara za ndani kilomita 275.9, mradi wa ujenzi wa barabara za mjini kilomita 103.7 pamoja na mradi wa ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 200. Barabara nilizozitaja hapo juu utekelezaji wake utafanyika kupitia miradi minne niliyoitaja.

**MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA BARABARA**

a. **Mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba.**

42. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imepanga kujenga barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba ili kuwaondoshea wananchi changamoto ya usafiri iliyopo hivi sasa katika maeneo mbalimbali ya mjini na vijijini. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya ASER na IRIS kutoka nchini Uturuki. Wizara imekamilisha maandalizi ya ujenzi wa barabara hizo na kazi inayoendelea ni kuzifanyia usanifu wa michoro barabara zilizopendekezwa katika mradi huo. Kazi ya usanifu wa michoro imekamilika kwa barabara ya Kibonde Mzungu –

Mwera kilomita 6.1, Dimani Sokoni – Dimani Beach kilomita 1.5, Kombeni – Nyamanzi kilomita 1, Jumbi – Chuo cha Utumishi (IPA) – Tunguu (Ringroad) kilomita 5, Kidimni – Ubago kilomita 4.3, Jumbi Sokoni – Kibondeni Skuli - Hospitali kilomita 4.4, Mgeni Haji – Kwambani kilomita 2.4 pamoja na barabara ya Cheju – Kibele kilomita 4.1. Aidha, Barabara ya majaribio kutoka Kibonde Mzungu hadi Mwera yenye urefu wa kilomita 6.1 tayari ujenzi wake umeanza. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya TSH 18,536,160,000 zimepatikana ikiwa ni malipo ya awali (Advance payment) ya Mkandarasi kwa mujibu wa Mkataba. Orodha ya Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba zinaonekana katika **kiambatanisho namba 3.**

**b. Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu Kilomita 125.6**

**43. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara kuu za Unguja na Pemba zikiwemo Tunguu – Makunduchi kilomita 48, Fumba – Kisauni kilomita 12, Mkoani - Chake Chake kilomita 43.5 pamoja na barabara ya Chake – Wete kilomita 22.1. Kwa upande wa barabara ya Tunguu – Makunduchi, Fumba – Kisauni na Mkoani - Chake Chake, Wizara imekamilisha kazi ya Upembezi Yakinifu, Usanifu na Uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za upatikanaji wa Mkopo wa fedha za ujenzi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mkandarasi ambae ni Kampuni ya PROPAV kutoka nchini Hispania. Kwa hatua ya awali, rasimu ya Mkataba tayari imeshapitiwa na pande zote mbili ambapo mara tu baada ya kukamilika hatua za upatikanaji wa Mkopo, Mkataba huo utakamilishwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

44. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Barabara ya Chake - Wete, Wizara imepanga kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya mradi wa barabara tatu za vijijini katika Mkoa wa Kaskazini Pemba uliojumuisha barabara ya Wete – Konde na Wete – Gando ambazo ujenzi wake umeshakamilika. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka BADEA na SAUDI FUND ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya MECCO kutoka Dar -es – Salaam. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi za ujenzi zimeanza kwa upimaji na usafishaji wa eneo la barabara lenye urefu wa kilomita 3.4 kuanzia Melitano hadi Ziwani Skuli.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 17,704,166,000, kati ya fedha hizo TSH 8,000,000,000 ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TSH 9,704,166,000 kutoka BADEA na SAUDI FUND. Hadi kufikia Machi, 2022, TSH 3,949,870,422 zimepatikana sawa na asilimia 22.3 ya makadirio ya bajeti. Aidha, kati ya fedha hizo, TSH 700,000,000 ni kutoka Serikalini na TSH 3,249,870,422 ni kutoka BADEA.

**c. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Jumbi - Sokoni - Tunguu (km 4.8)**

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuijenga Barabara ya Jumbi – Sokoni - Tunguu yenye urefu wa kilomita 4.8 kwa kiwango cha lami. Kazi inayoendelea hivi sasa ni kutayarisha zabuni ili kazi ya ujenzi wa barabara hiyo iweze kuanza.

**e. Upembuzi Yakinifu wa Daraja la Uzi Ng'ambwa (km 2.2)**

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kulijenga Daraja la Uzi Ng'ambwa ili kuwawezesha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kupata huduma za usafiri kwa urahisi zaidi. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kazi ya Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina (Detailed Design) na Uandaaji wa Michoro imekamilika kwa asilimia 100 na Mshauri Elekezi tayari ameshawasilisha ripoti yake Wizarani. Hata hivyo, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya michoro ya daraja hilo kwa lengo la kuangalia upya gharama za ujenzi wa daraja hilo ili kulijenga kwa gharama nafuu.

**f. Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mjini Kilomita 103.7**

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuzijenga barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 103.7. Mradi huu utahusisha uwekaji wa tabaka la juu la lami, njia za waenda kwa miguu, taa za kuongozea gari, taa za barabarani pamoja na misingi ya maji. Kazi ya kuandaa "concept design" pamoja na rasimu ya mkataba wa ujenzi imekamilika. Aidha, mradi huu utatumia njia ya usanifu na ujenzi (design and build) katika utekelezaji wake. Hivi sasa, kazi ya kuandaa makisio pamoja na mahitaji ya ujenzi wa barabara hizo inaendelea. Orodha ya Barabara hizo zinaonekana katika **kiambatanisho namba 4.**

**g. Mradi wa Ujenzi wa Barabara zenye Urefu wa Kilomita 200**

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuzijenga barabara mbalimbali zenye urefu wa kilomita 200. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za mjini, vijijini na barabara kuu ambazo hazijapata ufadhili. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Afisi ya Rais Fedha na Mipango tayari

imeshawasilisha maombi ya kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizo katika Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT. Orodha ya barabara hizo zinaonekana katika **kiambatanisho namba 5**.

**MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA ANGA**

**a. Mradi wa Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba**

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuutanua na kuuongezea miundombinu ili kuwezesha kutua ndege kubwa na kutumika wakati wote. Wizara inaendelea kutafuta fedha za ujenzi ambapo mazungumzo yanaendelea kwenye Kamati ya Madeni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutafuta fedha hizo kutoka kwa Mfadhili. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu na gharama za ujenzi zinaendelea na zitawasilishwa hivi karibuni.

**b. Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi.**

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Nungwi kwa kuutanua na kuuongezea miundombinu ili kuuwezesha kutua ndege aina ya Code C na kutumika wakati wote. Vile vile, Wizara ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kujenga jengo la zimamoto, kuvuta umeme, kujenga ofisi ya meneja, kujenga jengo la muda kwa ajili ya kuhudumia abiria wanao ondoka na wanao wasili pamoja na kuweka alama za kuongozea ndege katika Uwanja huo. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya utayarishaji wa michoro ya kina pamoja na kuendeleza ujenzi wa uzio katika uwanja huo. Pia, tayari eneo lenye urefu wa mita 2,200 na upana wa mita 200 limeshapimwa na mazungumzo ya kuongeza eneo lenye

urefu wa mita 3,000 na upana wa mita 1,000 yanaendelea. Kuwepo kwa Uwanja huu utausaidia Uwanja wa AAKIA pale panapotokea dharura za kiufundi na kiusalama.

52. **Mheshimiwa Spika,** uwanja huu tayari umeshaanza kutumika na ndege ndogo za aina ya Code D ikiwemo Caravan 2, Cessna 208, Let 410 na B E –20 tayari zimeanza kutua katika uwanja huo. Aidha, uwanja huu pia unatumika kwa shughuli za kitalii kama vile Sky diving.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 8,000,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2022, TSH 439,000,000 sawa na asilimia 5.4 zimetumika kwa ajili ya kujenga uzio katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA ambao tayari umekamilika.

**MRADI WA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA BAHARINI**

**a. Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani**

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kujenga Bandari Jumuishi Mangapwani inayojumuisha bandari ya Mafuta na Gesi, Bandari ya Mizigo na Chelezo kwa lengo la kuimarisha huduma za bandari ili kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia sekta ya usafiri wa bahari. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkuu (Master Plan) wa Bandari ya Mangapwani uliojumuisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya eneo hilo. Kwa sasa tayari Wawekezaji kadhaa wameshajitokeza kwa kuonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo. Mpango Mkuu huo, umeainisha maeneo yatakayojengwa bandari mbalimbali pamoja na mahitaji mengine muhimu ikiwemo miundombinu ya barabara, umeme, maji safi na maji machafu. Kwa upande wa Serikali inaendelea na kazi ya kumtafuta mkandarasi kwa

ajili ya kujenga miundombinu ikiwemo ya barabara katika eneo la bandari, umeme pamoja na miundombinu mengine inayohitajika. Hatua hii itaongeza kasi ya kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza katika bandari hii.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 3,000,000,000 kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya TSH 1,150,000,000 zimetumika sawa na asilimia 38 kwa ajili ya kumlipa Mshauri Elekezi kwa kuandaa Mpango Mkuu wa bandari hiyo.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 132,795,166,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 16,804,166,000 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 115,991,000,000 ni mchango kutoka Serikalini.
Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 35,895,425,604 zimetumika sawa na asilimia 27 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSH 10,857,680,707 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo sawa na asilimia 64.6 ya makadirio, TSH 25,037,744,897 ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 28 ya makadirio.

## MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa upande wa miradi ya maendeleo imepanga kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa katika Sekta ya Usafirishaji itakayogharimu jumla ya TSH 564,007,000,000. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara mbalimbali Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 501.5 ikiwemo barabara ya Mkoani – Chake

Chake kilomita 43, Fumba – Kisauni yenye urefu wa kilomita 12 na Barabara ya Tunguu – Makunduchi yenye urefu wa kilomita 48.5. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kuanza Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja na maandalizi ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani. Orodha ya miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inaonekana katika **kiambatanisho namba 6**.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya TSH 564,007,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## C.2. PROGRAMU YA PILI: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

59. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA, ambazo zinachangia ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

### C.2.1 Programu Ndogo ya Kwanza: Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA.

60. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) ambayo imepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Mkonga wa Mawasiliano wa Zanzibar, Kusimamia Kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa za Serikali pamoja na Minara ya

mawasiliano ya simu. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu bora ya Mawasiliano iliyo salama na endelevu.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA imeendelea na kazi zake za kawaida za matengenezo ya Mkonga katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja, matengenezo ya Mkonga yalifanyika katika njia ya Mwanakwerekwe Toronto hadi Makaburini. Matengenezo hayo yanatokana na uharibifu uliotokea wa kupigwa na radi Mkonga huo. Vilevile, matengenezo ya Mkonga yalifanyika katika eneo la Kizimkazi kutokana na kuwepo kwa matengenezo ya Barabara katika eneo hilo. Pia, katika eneo la Chuo cha Ualimu Nkurumah matengenezo yalifanyika baada ya Mkonga kukatika kutokana na ujenzi wa Hoteli ya Verde na katika eneo la Mkokotoni ambapo uharibifu wake umetokana na hujuma za makusudi za wananchi.

62. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, matengenezo yalifanyika katika njia (route) ya Gamba hadi Matemwe na eneo la Tunguu - SUZA ambapo matengenezo hayo yalitokana na Mkonga kuliwa na Panya, pamoja na eneo la Skuli ya SOS kwa kukatika kwa Mkonga ulioharibika (kuoza).
Aidha, matengenezo ya Mkonga yalifanyika katika njia ya Fumba baada ya Mkonga kukatwa na gari la mizigo. Hii imetokana na mwendelezo wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Fuoni - Kombeni. Pia matengenezo yaliendelea katika mtaa wa Lumumba ambapo kukatika kwa Mkonga huo ulitokana na kubadilisha njia (route) ili kupisha ujenzi wa hospitali mpya. Aidha, katika maeneo ya Pwani Mchangani na Mkokotoni ambapo kukatika kwa Mkonga huo kulitokana na hujuma za makusudi za wananchi waliokuwa wakichimba mashimo katika maeneo hayo.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Pemba, Matengenezo ya Mkonga yamefanyika katika eneo la Gombani ambapo marekebisho ya Mkonga unaoiunganisha ZMUX yalifanyika. Vile vile matengenezo yalifanyika katika eneo la Ole Kipangani kwenye Mkonga unaounganisha Mji wa Chake Chake na Wete. Pia matengenezo yaliendelea katika eneo la Mkoani ambapo sababu ya matengenezo hayo ni kukatika Mkonga baada ya kuegemewa na tawi la mti. Vile vile, matengenezo ya Mkonga yaliendelea katika muunganiko wa Pemba mpaka Tanga baada ya nguzo zilizobeba Mkonga huo kuanguka. Matengenezo mengine yaliyofanyika kwa kukatika Mkonga unaofikisha huduma katika Ofisi ya Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) Mkoani.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, ZICTIA imeweza kusambaza takribani kilomita 600 za mkonga Unguja na Pemba, kati ya hizo wastani wa kilomita 50 zimesambazwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. Lengo la kuongeza urefu wa usambazaji wa Mkonga ni kutanua matumizi ya Mkonga Zanzibar ili kurahisisha huduma za mawasiliano.

65. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, ZICTIA imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya uwelewa juu ya utunzaji wa siri katika sehemu zao za kazi pamoja na mafunzo juu ya uelewa wa upimaji wa utendaji kazi kazini. Aidha, ZICTIA imewapatia mafunzo ya muda mfupi jumla ya Wafanyakazi 13 kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na kuleta ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

66. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, ZICTIA pia ilipata fursa ya kushiriki katika Tamasha la Nane (8) la Biashara lililofanyika katika viwanja vya Maisara, mwezi Januari, 2022 ambapo kupitia Tamasha

hilo ZICTIA iliweza kutoa uelewa kwa jamii juu ya Majukumu na kazi zinazofanywa na ZICTIA pamoja na kutoa elimu juu ya masuala ya Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar na Kituo cha Kuhifadhia Taarifa za Kielektroniki (Data Centre) kwa umuhimu wake na kwa maslahi mazima ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

67. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Mashirika, Mamlaka na Taasisi nyengine zinazojitegemea zinaanza kulipia huduma ya matumizi ya Mtandao (Internet), ZICTIA ilianza na hatua ya uwasilishaji wa rasimu ya mkataba kwa ajili ya kuipitia na kuwasilisha maoni yao ili kuwa na mkataba mmoja utakaotumika katika utekelezaji wa huduma hiyo ambapo baadhi ya Taasisi zilishawasilisha maoni hayo na kuyafanyia kazi. Aidha, Mkataba huo uliwasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupokea maoni juu ya mkataba huo. Vilevile, ZICTIA iliendelea na hatua ya kuwasilisha bei ya huduma ya mtandao na fomu za maombi zinazotaka kila Taasisi kuchagua na kujaza kasi (Bandwidth/ Capacity) zinazohitajika na kuanza kulipia mara tu baada ya kusaini Mkataba huo.

68. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA kupitia Washauri elekezi imekamilisha kazi ya uandaaji wa Upembuzi Yakinifu wa huduma zinazotolewa pamoja na Mpango Mkakati wa kibiashara. Hii imetokana na azma ya ZICTIA kufanya mageuzi kutoka Wakala na kuwa Shirika la Mawasiliano Zanzibar ambapo kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2021 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma inayoelekeza juu ya sharti la uwepo wa nyaraka hizo katika kulifanikisha suala hilo. Aidha, ZICTIA tayari imeshawasilisha Nyaraka hizo Afisi ya Rais, Fedha na Mipango na kupata baraka za kuendelea na hatua za kuwasilisha Waraka wa mageuzi husika katika Kamati ya Makatibu Wakuu.

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, ZICTIA imeendelea na kazi za kuziunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Taasisi za Serikali Unguja na Pemba ambapo jumla ya Taasisi arobaini na moja (41) zimeunganishwa. **Kiambatanisho namba 7A** kinahusika.

70. **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, ZICTIA imeendelea na uimarishaji wa huduma katika vituo vyake (POP) kwa kuzifanyia maboresho (services) jumla ya viyoyozi (AC) 37 Unguja na viyoyozi (AC) 11 Pemba. Kazi hii imejikita kwa vituo vya Mkonga (Sites) 15 kwa Unguja na Pemba. Vile vile, katika uimarishaji wa (POP), jumla ya majenereta 9 yamefanyiwa matengenezo (service) katika vituo vya Mkonga; vituo 8 kati ya hivyo ni vya Unguja na kituo 1 ni cha Pemba.

71. **Mheshimiwa Spika,** mbali na kazi ya kuendelea kuziunganisha Taasisi zote za Serikali na Mkonga wa mawasiliano wa Zanzibar na kuzipatia huduma tofauti ikiwemo mtandao (Internet na Intranet), ZICTIA kwa kushirikiana na Kampuni ya Zantel imekamilisha kazi ya kuiunganisha na mkonga Minara 63 ya kampuni hiyo ili kurahisisha huduma za mawasiliano.

72. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA imefanikiwa kuziunganisha na Kituo cha Kuhifadhia Taarifa (Data Centre) jumla ya taasisi mpya 7 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022. **Kiambatanisho namba 7B** kinahusika.

73. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Uimarishaji wa kituo hicho cha kuhifadhia taarifa baada ya kusaini mkataba na Mkandarasi (Softnet Technologies Limited) anaefanya kazi hiyo na utekelezaji wa mradi huo ulianza kwa kuwapatia mafunzo elekezi wataalamu wa ZICTIA yatakayowaongezea ujuzi hususan katika matumizi ya teknolojia mpya itakayowekwa. Aidha, kwa

sasa ZICTIA imeshapokea vifaa vyote muhimu kutoka kwa Mkandarasi na vimeshafungwa katika kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center). Kazi inayoendelea sasa ni kuhamisha taarifa zilizopo kwenda kwenye vifaa vipya vilivyofungwa (Installation, Configuration, Testing, Migration of existing data). Kituo hicho kitakuwa cha kwanza nchini chenye hadhi ya "Software Defined" ambapo utekelezaji wa mradi huo hadi kukamilika kwake unakadiriwa kutumia jumla ya TSH 4,085,612,000 ambapo hadi sasa ZICTIA imeshapokea jumla ya TSH 2,000,000,000 sawa na asilimia 50 ya makadirio, ikiwa TSH 1,000,000,000 zimeingizwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 na TSH 1,000,000,000 katika mwaka wa fedha 2021/2022 na TSH 1,458,138,515 kati ya hizo zimetumika sawa na asilimia 40 ya malipo ya Mkandarasi kwa mujibu wa Mkataba.

74. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mapato, ZICTIA kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ilikadiriwa kukusanya jumla ya TSH 1,758,602,250 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 2,291,981,194 zimekusanywa sawa na asilimia 130 ya makadirio kwa kipindi husika.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,210,500,000 ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida na Mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 1,686,507,779 zimetumika sawa na asilimia 76.3 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, jumla ya TSH 389,455,835 ni Mshahara na TSH 1,297,051,944 ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo TSH 1,000,000,000 zimetumika kwa ajili ya mradi wa kuimarisha kituo cha kuhifadhia kumbukumbu (Data Center).

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.**

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA imepanga kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa Taasisi hii kutoka Uwakala kwenda kwenye mfumo wa Shirika kutokana na kuwa mfumo wa kiuendeshaji wa Uwakala uliopo hivi sasa hautoi fursa katika kukuza huduma za Mawasiliano. Wizara kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA imeshakamilisha Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) pamoja na Mpango wa Biashara (Strategic Business Plan) ikiwa ni matakwa ya Sheria nambari 6 ya mwaka, 2021 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma inayotaka kabla ya kuibadili taasisi kuwa Shirika kunahitajika kuwepo Upembuzi Yakinifu pamoja na Mpango wa Biashara na tayari taarifa hizo zimeshawasilishwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na imeonekana inafaa na kuleta tija kuibadili Taasisi hiyo.

77. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA imepanga kukamilisha mradi wa uimarishaji kituo cha kutunzia taarifa na kuwa kituo cha kwanza nchini chenye hadhi ya "Software Define" ili kuimarika kwa usalama taarifa zinazohifadhiwa pamoja na kuwahakikishia wateja (Taasisi) juu upatikanaji wa huduma bora za "Data Center".

78. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA imepanga kuifanyia mabadiliko Sheria nambari 15 ya mwaka 2020 ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji katika Sekta ya Mawasiliano. Sheria hiyo itaiwezesha ZICTIA kwa kushirikiana na wawekezaji hao kuwekeza katika Miundombinu ya TEHAMA ya Kimkakati ikiwemo kuweka njia ya Mkonga wa Kimataifa wa Baharini (International

Gateway). Hali hii itasaidia kuongeza vivutio kwa wawekezaji katika sekta mbalimbali pamoja na kupunguza bei ya mtandao nchini.

Pia, ZICTIA kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) inaendelea na mchakato wa kuandaa Mji wa TEHAMA ambapo wawekezaji wakubwa wote ikiwemo wawekezaji wa "Technology Park" inayojumuisha Kituo cha kukuza ubunifu (ICT Hub) ambapo wataalam wa TEHAMA na Ofisi mbalimbali za Kampuni za TEHAMA zitawekeza.

Aidha, ZICTIA imepanga kuanza ukusanyaji wa mapato yanayotokana na minara ya mawasiliano ikiwa ni agizo la Serikali la kutaka jukumu hili kusimamiwa na ZICTIA, ambapo hapo awali ada za minara ya mawasiliano zilikuwa zinakusanywa na Halmashauri kupitia Mawakala.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara kupitia Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imepangiwa kukusanya jumla ya TSH 3,029,000,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Aidha, Wakala imepangiwa kutumia jumla ya TSH 2,365,100,000 ambazo ni Ruzuku kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

**C.2.2. Programu Ndogo ya Pili: Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.**

80. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya pili ya usimamizi wa huduma za TEHAMA inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yanaongezeka kwa Taasisi zote pamoja na jamii.

81. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Wizara kupitia programu hii imeendelea

kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, intaneti pamoja na huduma za TEHAMA. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano imetoa mafunzo ya TEHAMA Unguja na Pemba kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii vilivyopo katika kila Wilaya. Mafunzo hayo yalikuwa yakihusiana na Uraia wa Kidijitali (Digital Citizenship) na kuwahusisha wananchi mbalimbali wakiwemo masheha na vijana. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwafanya wananchi wawe na uwelewa wa mambo ya msingi katika utumiaji sahihi wa kompyuta pamoja na kuongeza wigo katika matumizi ya TEHAMA ili waweze kujiendeleza na kujiajiri kupitia programu hizo.

82. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, jumla ya wananchi 2,179 wamepata mafunzo na huduma mbalimbali zinazotolewa katika vituo hivyo. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza kazi hiyo ya kutoa mafunzo kupitia kituo chengine cha TEHAMA kinachoendelea kujengwa Wilaya ya Magharibi "B" katika Skuli ya Bwefum.

83. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) imefanikiwa kujenga kituo na kuweka mifumo ya Mawasiliano ya Dharura (Emegency Call Center) katika eneo la Kiembe Samaki ambapo namba 190 inatumika kwa kupiga simu endapo pakitokea dharura yeyote nchini. Aidha, kwa kupiga namba hiyo, wananchi wataweza kuripoti taarifa mbalimbali zinazohusiana na maafa ikiwemo moto, afya na taarifa nyengine zinazohusiana na maafa au majanga mengineyo. Mradi huu wa Kituo cha mawasiliano ya Dharura Zanzibar (Zanzibar Emergency Call Center) umekamilika na kukabidhiwa rasmi mnamo tarehe 07 Machi, 2022.

84. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu Operesheni ya Anuani za Makaazi kufuatia agizo la tarehe 08 Fubruari, 2022 lililotolewa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kila Mtanzania apate anuani ya makaazi. Hadi sasa, jumla ya Anuani za Makaazi 499,787 katika Shehia zote 388 za Unguja na Pemba zimetolewa na kuchukuliwa taarifa za makaazi pamoja na kusajiliwa katika mfumo wa National Physical Addressing (NaPA).

85. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinafika na zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilifanya ukaguzi katika maeneo yote Unguja na Pemba na kubaini maeneo kadhaa ambayo yana matatizo ya mawasiliano ambapo baadhi ya maeneo, mawasiliano yake ni dhaifu (Weak signal) na mengine hayana mawasiliano kabisa. Baada ya ukaguzi na kupata matokea hayo kutoka TCRA, Wizara iliwataarifu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ili waweze kusaidia kutatua changamoto hizo. Hivyo, UCSAF ilichukuwa hatua ya kuondosha changamoto hiyo kwa kuingia Mkataba na Kampuni binafsi ya Zantel kujenga minara 42 katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba. Tayari Kampuni ya HTT Infraco Limited ambayo imepewa jukumu hilo la ujenzi inaendelea na ujenzi wa minara hiyo katika maeneo yote yaliyopendekezwa kwa Unguja na Pemba. Jumla ya vijiji 80 Unguja na Pemba vitafaidika na mradi huo baada ya kukamilika kwa ujenzi wa minara hiyo. Mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto ya mawasiliano katika maeneo hayo. Hadi sasa jumla ya minara 30 imekamilika ujenzi wake na minara 12 inaendelea na ujenzi katika hatua mbalimbali. **Kiambatanisho namba 8** kinahusika.

**86. Mheshmiwa Spika,** mbali na minara hii 42 inayojengwa kupitia msaada wa fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kampuni za simu za Zantel, TTCL na Halotel zimejenga na zinaendelea na ujenzi utakaojumuisha jumla ya minara 30 Unguja na Pemba.

**87. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Mawasiliano ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,304,275,000 kwa matumizi ya kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, TSH 326,048,397 zimetumika sawa na asilimia 25 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 194,486,240 ni Mishahara na TSH 131,562,157 ni kwa kazi za kawaida.

## MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

**88. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mawasiliano inaendelea kuratibu huduma mbalimbali za mawasiliano kama vile posta, simu na intaneti pamoja na kuendelea kutoa huduma na mafunzo ya TEHAMA kwa jamii kupitia Vituo vya TEHAMA jamii vilivyopo katika Wilaya za Unguja na Pemba. Aidha, Idara inatarajia kujenga vituo vyengine ili kuwafikia wananchi wengi kwa wakati mmoja na kwa ukaribu zaidi. Vilevile, Idara imepanga kuanzisha mfumo utakaowezesha kuwaunganisha, kuwatambua na kuwasajili wafanyakazi wote wenye taaluma ya TEHAMA waliopo Serikalini kwa lengo la kuwajengea uwezo kila panapotokezea mabadiliko ya TEHAMA ili kufanya kazi zao bila ya vikwazo. Aidha, kuwepo kwa mfumo huo kutasaidia kupata takwimu sahihi za wataalamu na hatimae kutoa mapendekezo Serikalini ya kuwapangia kazi kutokana na taaluma walizonazo.

89. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepanga kutengeneza mfumo utakaosaidia kuziunganisha Taasisi zake zote ili kuleta ufanisi wa kazi pamoja na kuunganisha baadhi ya mifumo yao na mfumo wa Wizara. Mfumo huu utasaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo utaoji wa ripoti mbalimbali za kiutendaji. Vilevile, Idara imepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya mda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi na weledi kulingana na mabadiliko ya teknolojia. Aidha, Idara imepanga kuandaa Mpango Mkuu wa TEHAMA Zanzibar (Zanzibar ICT Master Plan) kwa lengo la kuwa na mwelekeo sahihi katika kusimamia sekta ya mawasiliano Zanzibar.

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mawasiliano imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,091,540,000 kwa matumizi ya kawaida na mishahara.

## C.3. PROGRAMU YA TATU: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI.

91. **Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni; Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

### C.3.1. Programu Ndogo ya Kwanza: Utawala na Uendeshaji.

92. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo imepewa jukumu la kusimamia uendeshaji wa Wizara na kushughulikia

maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inasimamia na kuandaa Mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za wafanyakazi na mali za Wizara.

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi zilizofanyika chini ya programu hii ndogo ni kuwajengea uwezo Wafanyakazi 26 kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi. **Kiambatanisho namba 9A na 9B** kinahusika.

Pia, katika kuhakikisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa watendaji yanaimarishwa, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imezifanyia matengenezo ofisi mbalimbali, kuimarisha vitendea kazi kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao nyengine ikiwemo malipo ya likizo na malipo baada ya saa za kazi. Mbali na hayo, Idara imeufanyia mapitio Mpango wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi wa Wizara kwa lengo la kuwa na utaratibu bora wa kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

94. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,310,366,000 kwa kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2021, TSH 1,074,150,058 zimetumika sawa na asilimia 47 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 787,475,847 ni Mishahara na TSH 286,674,211 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

95. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kuwajengea

uwezo wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi pamoja na kuimarisha huduma za kiutawala na utumishi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi. Aidha, Idara imepanga kukamilisha Mpango wa Mahitaji ya Taasisi (Capacity Need Assessment) na kuandaa Mpango wa Mafunzo kwa watendaji.

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepangiwa kutumia jumla ya TSH 2,618,597,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

**C.3.2. Programu Ndogo ya Pili: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.**

97. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti pamoja na miradi ya maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji.

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea kusimamia na kuratibu miradi mbalimbali ya maendeleo, kukusanya takwimu mbalimbali katika sekta za usafiri wa nchi kavu, anga na baharini pamoja na kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara. Aidha, Wizara imeanza kuifanyia mapitio Sera ya Taifa ya Usafiri ya mwaka 2008 kwa lengo la kufanya matayarisho ya uandaaji wa Sera mpya ya Usafiri Zanzibar itakayoendana na wakati tulionao ambayo kazi hiyo inaendelea na ipo katika hatua za awali.

**99. Mheshimiwa Spika,** Idara pia inaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika mbalimbali yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na kuratibu na kuandaa vikao viwili vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - SMT na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - SMZ vinavyohusu Sekta ya Uchukuzi. Vikao hivi vimesaidia sana katika kubadilishana uzoefu wa kazi pamoja na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zinaikabili sekta ya Usafirishaji.

Vilevile, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kuwajengea uwezo watendaji wake na wale wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuwapatia mafunzo yanayohusiana na utayarishaji wa bajeti inayotumia mfumo wa PBB kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar. Aidha, Idara imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wake kuhusiana na usimamizi wa miradi.

**100. Mheshimiwa Spika,** Mnamo mwezi wa Machi, 2019, Shirika la Bahari Duniani (IMO) liliifanyia ukaguzi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na Usafiri wa Baharini. Miongoni mwa maeneo yaliyokaguliwa ni Wajibu wa Nchi zenye Bandari (Port State Control), Wajibu wa Nchi zenye Mwambao (Coastal State Control), Wajibu wa Nchi zenye Meli za Kimataifa (Flag State Responsibilities) pamoja na maeneo ya ujumla. Kwa upande wa Zanzibar, Ukaguzi huo ulibaini kasoro mbalimbali ambazo Serikali ilitakiwa kuzifanyia marekebisho kasoro hizo ili tuweze kuenda sambamba na Mikataba ya Kimataifa ya Usafiri wa Bahari inayotolewa na Umoja wa Maitaifa kupitia Shirika lake la kusimamia Usafiri wa Bahari (IMO) pamoja na kuimarisha huduma za usafiri wa bahari. Miongoni mwa kasoro hizo ni kuwepo kwa mapungufu makubwa katika Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006, kuwepo kwa upungufu wa taaluma

ya Usafiri Bahari kwa watendaji pamoja na kukosekana kwa mifumo thabiti ya usimamizi wa meli zetu za kimataifa. Hivyo, Wizara tayari imeshaifanyia marekebisho Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006 na sasa ipo katika hatua za kuwasilishwa katika vikao mbalimbali kwa mujibu wa utaratibu wa Serikali wa uandaaji wa sheria kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Aidha kwa upande wa kasoro nyengine, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ipo katika hatua za kuzifanyia kazi kasoro hizo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri Baharini pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar.

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 801,336,000 kwa kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia Machi, 2022, TSH 336,805,929 zimetumika sawa na asilimia 42 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 200,598,295 ni mishahara na TSH 136,207,634 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.**

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kuendelea kuratibu na kufanya Tafiti za Wizara, kuzifanyia mapitio Sera ya Usafiri ya mwaka 2008 na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013 ili ziendane na mahitaji ya sasa pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara ili uendane na Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo. Vilevile, Idara imepanga kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu mbalimbali katika sekta zinazosimamiwa na Wizara, kutayarisha Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa kazi za Wizara (Monitoring and Evalution Frame Work), kuratibu Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara, kuratibu na kufanya

vikao vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMT) pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT). Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wake yanayohusiana na utayarishaji wa bajeti katika mfumo wa programu (PBB), ufuatiliaji na tathmini, namna ya kufanya tafiti pamoja na usimamizi wa miradi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,030,728,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

### C.3.3. Programu Ndogo ya Tatu: Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

104. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo imepewa jukumu la uratibu wa kazi za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo kuratibu kazi za utawala na utumishi, kazi za mipango na bajeti, usimamizi wa ujenzi wa barabara mbalimbali ikiwemo Kipapo - Mgelema, Micheweni maeneo Huru pamoja na Barabara ya Chake - Wete yenye urefu wa kilomita 22.1 ambayo ujenzi wake umeanza rasmi, kusimamia huduma za usafiri na usalama barabarani, kusimamia huduma za mawasiliano ikiwemo huduma za TEHAMA pamoja na kusimamia anuani za makaazi na postikodi.

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi Kuu - Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya TSH

1,003,222,000 kwa kazi za kawaida na mishahara na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 387,179,925 zimetumika sawa na asilimia 38.6 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 237,179,925 ni mishahara na TSH 150,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida.

**MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**106. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi Kuu Pemba imepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuweka mazingira bora ya Ofisi kwa kufanya matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi lililopo Chake Chake. Aidha, Ofisi Kuu Pemba itaendelea kusimamia maslahi ya watumishi kwa kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa Sheria pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi.

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi – Kuu Pemba imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,040,954,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kupitia Programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliidhinishiwa na Baraza la Wawakilishi kutumia jumla ya TSH 147,595,566,000 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 43,622,865,413 zimetumika sawa na asilimia 29.5 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 35,895,425,604 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo na TSH 7,727,439,809 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ruzuku. **Kiambatanisho namba 10** kinahusika.

**UKUSANYAJI WA MAPATO**

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha

Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 4,335,056,750 na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 4,775,579,496 zimekusanywa sawa na asilimia 110 ya makadirio ya robo tatu. **Kiambatanisho namba 11** kinahusika.

## D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2021 HADI MACHI, 2022 PAMOJA NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

### D.1. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

**110. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inaendelea na kazi zake za msingi za kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama wa safari za abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati wa utekelezaji wa majukumu yake inazingatia taratibu na sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA) na International Civil Aviation Organization (ICAO).

**111. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

**a. Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba**.

**112. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa viwanja vya Ndege, Mamlaka imetoa mafunzo ya ulinzi na usalama kwa wafanyakazi 259 ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na uweledi zaidi. Aidha, Serikali imefanya

ununuzi wa mashine tano za ukaguzi wa mzigo ambazo tatu zitatumika katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA na mbili zitatumika katika Uwanja wa Ndege wa Pemba, mashine hizo tayari zimeshafika hapa Zanzibar na kazi ya kuzifunga (Installation works) inaendelea. Aidha, Mamlaka imeongeza kamera za ulinzi (CCTV) 35 katika maeneo yote ya ndani ya Uwanja yakiwemo maeneo yanayo kusanywa Mapato ili kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya viwanja. Kwa jumla, Uwanja wa Ndege wa AAKIA una Kamera 81 zinazofanya kazi kwa sasa na kwa Uwanja wa Ndege wa Pemba una jumla ya Kamera 21, kati ya hizo 6 zimewekwa katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

**b. Mradi wa Uwekaji wa Taa za Kuongozea Ndege (Precession Lights)**

**113. Mheshimiwa Spika,** Wizara ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iko katika hatua za mwisho za ununuzi kwa ajili ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege (Precession Lights) zitakazofanya kazi sambamba na mfumo wa kumuongoza Rubani (Instrument Landing System). Mradi huu utakapokamilika utamuwezesha rubani kutua katika uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa usalama zaidi hasa nyakati zile za mvua kubwa ambapo marubani hupata shida ya kutua ndege kutokana na hali ya hewa.

**c. Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA**

**114. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanikiwa kuimarisha mazingira ya biashara katika Uwanja wa AAKIA kwa kuingia Mkataba na Kampuni ya Emirates Leisure kutoka UAE kwa ajili ya kuimarisha na kuendesha huduma za maduka na migahawa kwa hadhi ya kimataifa. Kampuni hiyo

itatoa huduma hizo zitakazojumuisha bidhaa mbalimbali zikiwemo za kiasili. Aidha, Mamlaka imeingia makubaliano na kampuni ya DNATA kwa ajili ya uendeshaji wa kumbi za kibiashara (Business Lounge) pamoja na utoaji wa huduma za ndege (ground handling services). Kampuni hiyo tayari imeshaleta vifaa pamoja na kuanza kazi ya kufanya maboresho ya ukumbi huo.

**d. Uwekaji wa Mifumo Mbalimbali katika Uwanja wa Ndege wa Pemba.**

**115. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaimarisha huduma pamoja na ukusanyaji wa mapato katika Uwanja wa Ndege wa Pemba, inaendelea na uwekaji wa miundombinu ya mfumo wa kuwahakiki abiria, mfumo wa taarifa za ndege (Flight Information Display System) pamoja na mfumo wa maegesho ya gari katika Uwanja huo. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeweka geti (BoomGate) katika maegesho ya jengo la abiria la Terminal III na Terminal II ambayo yanatumika kwa ajili ya kudhibiti malipo ya maegesho ya vyombo vya moto kwenye maegesho hayo. Vilevile, taratibu za kuweka mageti hayo kwa upande wa Uwanja wa Ndege wa Pemba unaendelea.

**e. Kuongezeka kwa Mashirika ya Ndege yanayofanya Safari zake Zanzibar**

**116. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuimarika kwa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kumepelekea kuongeza mashirika mapya tisa (9) ya Ndege yanayofanya safari zake kuja Zanzibar. Mashirika hayo ni Air France, Eurowings, Edelweiss, Etihad na Global Airways ambayo yana ratiba maalum (schedule flights)

na kwa yale yasiokuwa na Ratiba Maalum (Non-Schedule flights) ni pamoja na Azur Ukrain, Hisky Europe, Europian Charter na Smart Wings. Mashirika hayo yamesaidia sana kuimarisha sekta ya utalii na biashara hapa Zanzibar.

### f. Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi Mbalimbali

117. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya viwanja vya Ndege imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 19 na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 207 katika kada tofauti ikiwemo, Usalama (security), Uegeshaji ndege, Kompyuta, Uhudumu, Uhusiano, Biashara, Uwekaji kumbukumbu, Utawala, Manunuzi, Sekretari, Mipango, Ufundi, Kujiandaa na kustaafu pamoja na mafunzo kwa vitendo.

### TAKWIMU ZA ABIRIA, MZIGO NA SAFARI ZA NDEGE

118. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka imehudumia jumla ya safari za ndege 36,554 ikilinganishwa na safari 32,660 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 12. Kati ya safari hizo, safari za ndege 32,650 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na safari za ndege 3,904 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Safari za ndege za Kimataifa zilikuwa ni 5,868 na safari za ndani zilikuwa ni 30,686. **Kiambatanisho namba 12A** kinahusika.

119. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeweza kuhudumia abiria 973,975 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ,ikilinganishwa na abiria 741,043 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 31. Abiria 907,837 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege

wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 66,138 walihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Kati ya abiria hao, abiria 545,067 wakiwa ni wa safari za kimataifa na 428,908 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit passengers) ni 110,917 ambapo 110,434 walipita katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 483 waliopita katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. **Kiambatanisho namba 12B** kinahusika.

**120.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mizigo, Mamlaka imehudumia jumla ya mzigo tani 2,106 katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ikilinganishwa na mzigo tani 1,689 katika kipindi kama hicho 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 25.

**121.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imehudumia jumla ya Mashirika na Kampuni za ndege zipatazo 47 za ndani na nje katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar. **Kiambatanisho namba 12C** kinahusika.

**MAPATO NA MATUMIZI**

**122.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kukusanya jumla ya TSH 19,193,536,541 kupitia vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya TSH 13,604,386,564 zimekusanywa sawa na asilimia 71 ya makadirio ya robo tatu.

**123.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kutumia jumla ya TSH 27,652,519,234. Kati ya fedha hizo, TSH 23,938,171,910 ni kwa kazi za kawaida na TSH 3,714,347,324, kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2021, jumla ya TSH 11,069,421,346 zimetumika sawa na asilimia 40 ya

makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TSH 5,309,836,129 mishahara na TSH 4,667,893,582 kwa ajili ya kazi za kawaida na TSH 1,091,691,635 kwa kazi za maendeleo.

## MALENGO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

124. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mamlaka imepanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuwapatia wafanyakazi 223 mafunzo ya ulinzi na usalama katika fani mbalimbali. Aidha, Mamlaka imepanga kulifanyia ukarabati jengo la abiria linalotumika sasa katika Uwanja wa AAKIA (Terminal Building II) na pamoja na jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Pemba. Vilevile, Mamlaka imepanga kufanya Upembuzi Yakinifu na Michoro ya kina kwa ajili ya ujenzi wa Jengo jipya la abiria (Terminal Building 4) ili kukabiliana na ongezeko la abiria kwa sasa na miaka 30 ijayo.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka imepanga kuondosha mabaki ya mipira ya ndege zinazotua na kuruka katika Barabara ya kurukia na kutulia ndege (runway) katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA pamoja na kufanya matengenezo ya barabara ya kupitia ndege (taxiway C) katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA ambayo imeharibika. Aidha, Mamlaka imepanga kuzifanyia matengenezo taa za kuongozea ndege na kuweka alama za kuongozea ndege katika maeneo ya barabara ya kurukia na kutulia ndege, njia za kupitia ndege (taxiways) na maegesho ya ndege (apron) katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA. Mamlaka imepanga kuendeleza Uwanja wa Ndege wa Nungwi kwa kuuwekea "beacon" katika maeneo yake yote yanayouzunguka uwanja huo, kujenga barabara inayouzunguka uwanja huo kwa ajili ya kufanyia doria pamoja na kulipa fidia kwa wananchi

watakaoathirika na uendelezaji huo.

Vilevile, Mamlaka imepanga kununua mabasi matatu kwa ajili ya huduma ya usafiri wa kuwapeleka na kuwarejesha kazini wafanyakazi wa Mamlaka pamoja na kuwapatia mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa Uwanja wafanyakazi wa Mamlaka. Aidha, Mamlaka imepanga kuhudumia abiria 1,782,834, Ndege 82,632 na Mzigo tani 3,410 kwa Unguja na Pemba.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023**

**125. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya TSH 34,000,520,866 kupitia vyanzo vyake vya ndani na imepanga kutumia jumla ya TSH 31,084,201,869. Kati ya hizo, TSH 21,155,962,869 kwa kazi za kawaida na 9,928,239,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

**D.2. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR.**

**126. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni za makampuni yanayojishughulisha na huduma za bandarini, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia pamoja na kuidhinisha (endorsement) vyeti vya mabaharia. Aidha, Mamlaka ina jukumu la kusimamia usalama wa bandari zilizopo Zanzibar ikiwa ni utekelezaji wa Kanuni na Miongozo ya Kimataifa na Kikanda, kudhibiti safari za vyombo vya baharini, uchunguzi wa ajali za baharini,

uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa ajali za baharini pamoja na usimamizi wa maslahi ya mabaharia.

127. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

**a. Kuufanyia mapitio Mpango Mkakati wa Mamlaka**

128. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022 Mamlaka imeufanyia mapitio Mpango Mkakati wa mwaka 2016/2021 unaotekelezwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa lengo la kuanza kutayarisha Mpango Mkakati mpya utakao kwenda sambamba na miongozo ya kitaifa na kimataifa inayotolewa na Shirika la Bahari Duniani (IMO).

**b. Kuzifanyia Mapitio Sheria, Kanuni na Miongozo.**

129. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka imeifanyia mapitio Sheria ya Usafiri Baharini (namba 5 ya mwaka 2006) na kuweza kuifanyia marekebisho Sheria hiyo na kwa sasa ipo katika hatua ya kuwasilishwa katika vikao mbalimbali Serikalini kwa mujibu wa taratibu za kuandaa Sheria kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Vile vile, Mamlaka imeifanyia marekebisho Kanuni ya ada na tozo ya mwaka 2012 na Kanuni hiyo tayari imeanza kutumika.

**c. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mamlaka**

130. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, ZMA imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 28 katika fani mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**d. Usajili wa meli**

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka ilisajili jumla ya meli 99 zenye uzito wa GRT 658,128. Kati ya meli hizo, meli 85 ni usajili wa meli za kimataifa zenye uzito wa GRT 641,351 na meli 11 ni usajili wa meli za ndani zenye uzito wa GRT 16,777.

**132. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba baada ya usajili wa meli za kimataifa kusimamishwa, kwa sasa Mamlaka ya Usafiri Baharini imeruhusiwa rasmi kuendelea na usajili meli hizo na kwa kipindi cha muda mfupi imesajili meli za kimataifa 85 na kuingiza jumla ya TSH 639,308,000. Hali hii itaiwezesha Mamlaka kuongeza mapato pamoja na kuitangaza Tanzania katika Sekta ya Usafiri wa Baharini.

**e. Kupatikana Mfumo wa Usajili wa Meli na Mabaharia kwa Njia za Kielektroniki**

**133. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanikiwa kuanzisha mfumo wa usajili wa meli za ndani na za nje kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unaosimamiwa na kampuni ya 'Ocean HQ Company Ltd' ya Uingereza. Kupitia mfumo huu, mmiliki wa meli ana uwezo wa kujaza fomu ya maombi kupitia tovuti ya ZMA na kuyatuma maombi hayo moja kwa moja na hivyo kuweza kufanyiwa kazi na Mamlaka kwa haraka. Mfumo huo unategemewa kusimamiwa na Mamlaka wenyewe mwishoni wa mwezi wa Juni, 2022. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kununua vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa kufuatilia meli zilizosajiliwa ndani na nje wakati zikiwa baharini (Electronic Ship Tracking System).

## f. Utoaji wa Leseni Mbalimbali Zinazohusu Shughuli za Usafiri wa Baharini

134. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Mamlaka imetoa leseni 501 kwa vyombo vidogo vidogo, leseni 330 za Manahodha, leseni nane (8) kwa Wahandisi (Boat Engineers), Vitabu vya Mabaharia (Discharge Books) 635 pamoja na mikataba 196.

Vilevile, Mamlaka imeidhinisha vyeti 81 vya mafunzo ya ulinzi melini (Security awareness) kwa Mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS, pamoja na kuthibitisha vyeti vya Mabaharia 347 (Endorsements) wa kigeni wanaofanya kazi katika meli zilizosajiliwa usajili wa kimataifa.

Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilitoa jumla ya leseni 118. Kati ya leseni hizo, 47 zimetolewa kwa Mawakala wa utoaji wa mizigo bandarini, leseni tatu (3) kwa ajili "Jetty Installation", leseni tisa (9) kwa vituo vya uzamiaji baharini, leseni tatu (3) kwa vyombo vya starehe, leseni saba (7) kwa vyombo vya michezo baharini, leseni saba (7) kwa kampuni zinazomiliki meli moja, leseni nne (4) kwa kampuni zinazomiliki meli zaidi ya moja, leseni tano (5) kwa mawakala wa meli za kigeni, leseni mbili (2) kwa michezo ya vishada baharini, leseni (10) kwa ajili ya mawakala wauza tiketi, leseni moja (1) kwa Kampuni zinazopiga dawa melini, leseni moja (1) kwa ukaguzi wa vifaa vya uzamiaji baharini, leseni mbili (2) kwa kampuni ya ukaguzi wa vifaa vya kuokolea maisha melini, leseni mbili (2) kwa ajili ya vifaa vya kuzimia moto melini, leseni (10) kwa Jet Ski, leseni mbili (2) kwa wamiliki wa meli, leseni mmoja (1) kwa wafungaji wa mizigo ya melini, na leseni mbili (2) kwa hoteli zinazoelea baharini.

**g. Ukaguzi wa Meli**

**135. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, Mamlaka ilikagua jumla ya meli 63 za ndani zenye jumla ya GRT 121,550. Kati ya meli hizo, meli 24 zenye jumla ya GRT 22,920 ziilfanyiwa ukaguzi wa kiusalama wa mwaka, meli saba (7) zenye GRT 8,152 zilifanyiwa ukaguzi wa dharura, meli 17 zenye GRT 19,630 zilifanyiwa ukaguzi wa kushtukiza, meli tisa (9) zenye GRT 7,462 zilifanyiwa ukaguzi wa chelezoni na meli sita (6) zenye GRT 63,385 zilifanyiwa ukaguzi wa awali.

**h. Usimamizi wa Uuzaji wa Tiketi za Meli na Boti za Abiria**

**136. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini inaendelea kulisimamia suala la ulanguzi wa tiketi kwa kuwaelimisha wananchi kupitia matangazo ya redio na Televisheni kuhusiana na ununuzi wa tiketi kwa kutumia kitambulisho. Mamlaka inafanya usimamizi na uhakiki kwa tiketi za abiria kwa mujibu wa vitambulisho vyao. Aidha, Mamlaka inawachukulia hatua wale wote wanaohusika na ulanguzi wa tiketi kwa kuwakamata na kuwapeleka katika vyombo vya Sheria. Kutokana na usimamizi huo, Mamlaka imeweza kupunguza ulanguzi wa tiketi kwa kiasi kikubwa. Jumla ya watu sita (6) wamekamatwa kwa kufanya ulanguzi wa tiketi na kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

**MAPATO NA MATUMIZI**

**137. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipanga kukusanya jumla ya TSH 3,502,412,000 hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 2,382,301,166 zimekusanywa sawa na asilimia 68 ya makadirio ya bajeti.

138. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kutumia jumla ya ya **TSH** 3,468,054,000. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 2,241,198,971 zimetumika sawa na asilimia 65 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 952,222,725 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya mishahara na TSH 1,288,976,246 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

139. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mamlaka imepanga kukamilisha mapitio ya Sheria pamoja na kutayarisha miongozo na kanuni mpya ili ziweze kuendana na matakwa ya Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Bahari Duniani (IMO), Aidha, Mamlaka imepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbalimbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uweledi. Vile vile, ZMA itaendelea kuzifanyia kazi hoja na mapungufu yatokanayo na ripoti ya ukaguzi wa IMO kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika. Aidha, mfumo wa kufuatilia meli na vyombo vidogo vidogo vilivyopo baharini (Monitoring Operation Center) nao utaanzishwa pamoja na kununua boti. Aidha, Mamlaka imepanga kuanza ujenzi wa Ofisi za Mamlaka Pemba.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023**

140. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla ya TSH 6,257,812,065 na imepanga kutumia jumla ya TSH 6,182,871,420 kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH TSH 5,837,871,420 kwa kazi za kawaida na TSH 345,000,000 kwa kazi za maendeleo.

### D.3 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR.

141. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, uangalizi wa alama za kuongozea meli (Minara na Maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini.

142. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Shirika limehudumia vyombo mbalimbali vya mizigo na abiria kupitia Bandari zake za Unguja na Pemba zikiwemo meli za kigeni, meli za ndani pamoja na majahazi, ambapo meli za kigeni zilizohudumiwa ni 95 zenye uzito wa GRT 1,145,671 ikiwa ni upungufu wa meli tano (5) sawa na asilimia tano (5) ikilinganishwa na meli 100 zenye uzito wa GRT 1,097,821 zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021.

143. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa meli za ndani, jumla ya meli 3,632 zilihudumiwa ikiwa ni ongezeko la meli 270 sawa na asilimia nane (8) ya meli za ndani 3,362 zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Aidha, jumla ya majahazi na boti za vyuma 8,181 yamehudumiwa katika kipindi hicho ikiwa ni ongezeko la majahazi 2,980 sawa na asilimia 59 ikilinganishwa na majahazi 5,201 yaliyohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Ongezeko hilo la majahazi linatokana na kuongezeka kwa mzigo wa saruji unaosafirishwa pamoja na bidhaa nyengine.

144. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika limehudumia jumla ya tani 719,630 za mzigo wa meli ikiwa ni ongezeko la tani 132,415 sawa na asilimia 23

ukilinganisha na tani 587,215 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Ongezeko hili linatokana na mizigo kuja kwa njia ya kichele badala ya makontena kulikosababishwa na athari za Uviko 19 ambapo kumekuwa na upungufu wa makontena matupu duniani. Aidha, jumla ya tani 209,927 za mzigo wa majahazi zimehudumiwa ikiwa ni ongezeko la tani 134,754 sawa na asilimia 179 ya tani 75,172 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022. Ongezeko la mzigo wa majahazi unatokana na usafirishaji wa saruji kutoka Tanzania bara pamoja na bidhaa nyengine.

Kwa upande wa makontena, jumla ya makontena 37,743 (sawa na TEUS 50,734) yamehudumiwa ikiwa ni ongezeko la makontena 1,306 (TEUS 1,979) sawa na asilimia 4 ya makontena 36,437 yaliyohudumiwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. **Kiambatanisho namba 13A na 13B** kinahusika.

**145. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Shirika linaendelea kuimarisha vifaa vya kufanyia kazi bandarini ili kuleta ufanisi wa kuhudumia mizigo na vyombo katika bandari zetu. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Shirika limeshasaini mikataba 12 na Kampuni mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi bandarini ambavyo ni Mizani 4, Reach stacker 1, Mobile harbor crane 1 ya tani 124, Mobile crane 1 ya tani 60, Trailer 1, terminal tractor 1, Empty reach stacker 1, Transformer 1, Spreder 4, Winch Trunk 1, Semi Teller 1pamoja na ununuzi wa Generator 1. Vifaa hivyo vinatarajiwa kupokelewa ndani ya kipindi cha robo ya kwanza cha mwaka wa fedha 2022/2023. Kupatikana kwa vitendea kazi hivyo kutaimarisha huduma za bandari, kuongeza mapato pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Bandari lilipanga kutumia jumla ya TSH 5,960,679,320 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo na hadi kufikia Machi, 2022 jumla ya TSH 375,519,200 zimetumika kwa malipo ya awamu ya kwanza (20%) ya ununuzi wa Reach stacker na Terminal Tractor.

**146. Mheshimiwa Spika,** Shirika limepanga kuimarisha Bandari ya Mkokotoni kwa kujenga Gati, barabara za ndani, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria, njia ya waenda kwa miguu pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel). Kwa upande wa ujenzi wa Gati ya Mkokotoni, ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, kwa kazi zilizobakia Shirika linaendelea kukamilisha taratibu za ufungaji wa mikataba kwa Kampuni tatu kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kazi hizo. Kampuni hizo ni Edge Engineering Consultant kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria pamoja njia ya waenda kwa miguu. Kampuni ya Coastal Dredging kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel) na Wakala wa Barabara kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya kuingilia Bandarini pamoja na eneo la ndani.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TSH 4,760,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na hadi kufikia mwezi wa machi, 2022, jumla ya TSH 2,417,388,590 zimetumika sawa na asilimia 50.8 ya makadirio kwa ajili ya ujenzi wa Gati ya Mkokotoni.

**b. Mradi wa Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani**

**147. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha matengenezo ya njia ya kupitia vyombo vya kutendea kazi bandarini, kujenga njia ya waendao kwa miguu, kuliimarisha eneo la kuwekea makontena, ujenzi wa uzio, ujenzi wa ukuta

wa kuzuia mmongonyoko, uwekaji wa "fender" pamoja na uwekaji wa zinc anode kuzuia kutu katika eneo la gati. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi iliyofanyika ni kukamilisha uwekaji wa "fender" kwa ajili ya kuegesha vyombo kwa usalama gatini katika bandari ya Mkoani. Vilevile, kwa kazi zilizobakia Shirika limekamilisha taratibu za ununuzi na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza ndani ya mwezi wa Mei, 2022.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,236,637,676 na hadi kuifikia Machi, 2022 jumla ya TSH 336,637,676 zimetumika sawa na asilimia ya 15 ya makadirio kwa ajili ya uwekaji wa Fenders.

**c. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini**

**148. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa Gati, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel). Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi iliyofanyika ni ulipaji wa fidia za mazao na vipando kwa wananchi wapato 19. Aidha, Shirika limekamilisha taratibu za ununuzi na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza ndani ya mwezi wa Mei, 2022.

Kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,170,630,000 na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022, jumla ya TSH 70,630,000 zimetumika sawa na asilimia 3 kwa ajili ya malipo ya fidia.

**d. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Wete.**

**149. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari imepanga kuifanyia Upembuzi Yakinifu bandari ya Wete kwa lengo la kuijenga upya bandari hiyo. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Shirika limekamilisha taratibu za ununuzi

na Kampuni ya INROS LACKNER kutoka nchini Ujerumani inatarajiwa kufanya kazi hiyo. Kazi ya Upembuzi Yakinifu inatarajiwa kuanza mwezi wa Juni, 2022. Kukamilika kwa kazi hiyo kutatoa fursa kwa Shirika kuendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo.
Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **TSH 160,000,000** kwa ajili ya malipo ya awali na hakuna fedha iliyotumika.

**e. Mradi wa Uimarishaji wa Bandari ya Malindi**

**150. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unajumuisha ukarabati wa majengo, uwekaji wa sakafu katika eneo la gati ya abiria, ukarabati wa eneo la kuhifadhia makontena pamoja na uchimbaji kwa ajili ya kuongeza kina cha maji katika Gati namba 3. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, kazi za ujenzi wa sakafu katika Gati ya abiria imekamilika na kazi zilizobakia zinaendelea. Mradi huu umefikia asilimia 30 ya utekelezaji.

**151. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TSH 750,000,000 na hadi kufikia Machi, 2022 jumla TSH 217,335,000 zimetumika sawa na asilimia 29 ya makadirio ya fedha zilizopangwa.

**f. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Kizimkazi.**

**152. Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea na hatua za awali za ujenzi katika bandari ya Kizimkazi. Kazi za upimaji wa eneo husika kwa ajili ya kufanya tathmini ya vipando, mazao na majengo zinaendelea na ripoti inatarajiwa kutolewa ndani ya mwezi wa Juni, 2022. Kutokana na umuhimu wa mradi huu na kuzingatia gharama zilizokadiriwa kufikia TSH 24,000,000,000, Shirika limekusudia kufanya Upembuzi Yakinifu katika mwaka wa fedha ujao.

**g. Uimarishaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Shirika la Bandari.**

**153. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuweka mfumo wa E - Port katika maeneo makuu matatu ambayo ni huduma za vyombo vya baharini, mizigo pamoja na utawala na uendeshaji wa Taasisi. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Shirika limefanikiwa kufunga Mkataba na Kampuni ya Wartsila Voyage Company Ltd association with Fortis Company Ltd kwa ajili ya kufanya kazi hiyo ambayo inatarajiwa kuanza robo ya mwisho ya mwaka 2021/2022. Mradi huu utakapokamilika utaliwezesha Shirika kuongeza mapato kwa kupunguza mianya ya upotevu wa mapato, kupunguza matumizi, kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati za Shirika pamoja na kurahisisha huduma kwa wateja. Kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Mradi huu umepangiwa jumla ya TSH 4,800,000,000 na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022 hakuna fedha iliyotumika.

**Mapato na Matumizi**

**154. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 42,317,368,347 na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 32,404,542,115 zimekusanywa sawa na asilimia 76.6 ya makadirio.
Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2021/2022 lilipanga kutumia jumla ya TSH 50,706,666,787 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2022, jumla ya TSH 18,092,569,379 zimetumika sawa na asilimia 35.7 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSH 10,974,879,047.63 ni matumizi ya kawaida, TSH 3,700,179,865.00 ni mishahara na TSH 3,417,510,467 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## MALENGO YA SHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

155. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limepanga kuhudumia jumla ya meli 145 za kigeni zenye uzito (GRT) wa tani 1,780,000, Meli za ndani zipatazo 4,700 na Majahazi 12,000. Aidha, kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika linatarajia kuhudumia tani 970,000 za mzigo mchanganyiko kwa meli za ndani na nje, makontena 64,540 (TEUs 86,543), tani 145,000 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel) pamoja na tani 355,000 za mzigo wa majahazi.

156. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2022/2023, limepanga kuendelea kukamilisha miradi inayoendelea ambayo ilianza utekelezaji wake ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwemo Bandari ya Mkokotoni, Bandari ya Shumba Mjini na Bandari ya Mkoani. Pia, Shirika limepanga kununua mizani mbili (2) zitakazotumika kupimia mizigo katika bandari ya Wete na Mkokotoni. Aidha, Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi 70 pamoja na mafunzo ya ndani 150.

### Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023

157. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika la Bandari Zanzibar limepanga kukusanya jumla ya TSH 53,770,651,303 na kutumia jumla ya TSH 58,924,448,630. Kati ya Fedha hizo TSH 39,802,505,057 kwa kazi za kawaida na TSH 19,121,943,572 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Shirika linategemea kutumia akiba ya ndani ya TSH 10,000,000,000 kwa ajili ya kufanikisha

miradi ya maendeleo pamoja na kuchukua Mkopo wa Jumla ya TSH 10,000,0000,000 ili kufanikisha miradi yake.

## D.4 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR.

**158. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar.

**159. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli linamiliki meli nne ambazo ni MV Maendeleo, MT Ukombozi, MV Mapinduzi II na MT Ukombozi II. Serikali imefanya maamuzi ya kuziuza meli zake mbili; meli ya abiria na mizigo MV Maendeleo na meli ya kuchukulia nishati ya mafuta MT Ukombozi. Meli hizi kwa sasa zimechakaa na gharama za uendeshaji wake ni kubwa kiasi ambacho hupelekea Shrika la Meli kupata hasara.

Kwa upande wa meli ya MV Mapinduzi II Serikali inakusudia kuikodisha, kuiendesha kwa pamoja na sekta binafsi (PPP) au kuiuza. Hatua hii imekuja kutokana na meli hii kuonekana kupata hasara tangu ilipoanza shughuli za usafirishaji mwaka 2016 kutokana na gharama za uendeshaji wake kuwa kubwa.

**160. Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea kutoa huduma za uwakala wa meli. Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya meli 267 za kigeni zimehudumiwa kwa kipindi cha miezi tisa.

**161. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa meli ya kuchukulia nishati ya mafuta ya MT Ukombozi II, kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, meli hii ilikodiwa kwa kodi ya safari (voyage charter) na Kampuni ya GBP Tanzania Limited. Meli imefanya jumla ya safari 21 kwa kipindi hicho na kuingiza jumla ya TSH 2,415,000,000.

**Mapato na Matumizi**

162. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 15,642,893,880 na hadi kufikia Machi, 2022, TSH 8,287,886,023 zimekusanywa sawa na asilimia 53 ya makadirio ya bajeti. Kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kunatokana na meli ya mafuta ya MT Ukombozi kusimama kufanya kazi ya kuchukua nishati ya mafuta kutokana na uchakavu.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TSH 11,740,173,679 kwa kazi za kawaida na maendeleo na hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 5,610,327,806 zilitumika sawa na asilimia 48 ya makadirio ya bajeti.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

163. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika limepanga kujenga meli mpya ya abiria na mizigo. Meli hiyo inatarajiwa kufanya safari zake baina ya visiwa vya Unguja na Pemba na maeneo mengine ya Mwambao wa Afrika Mashariki. Kwa upande wa Uwakala, Shirika limepanga kuhudumia jumla ya meli 267 zikiwemo za makontena, mizigo mchanganyiko, meli za gesi na meli za watalii.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023**

164. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika limepanga kukusanya jumla ya TSH 11,652,474,000 na kutumia jumla ya TSH 10,897,811,283 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya TSH 9,390,171,283 kwa kazi za kawaida na TSH 1,507,640,000 kwa kazi za maendeleo.

## E. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

**165. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Shirika la Posta la Tanzania (TPC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC). Mashirikiano na Taasisi hizo yamechangia sana kukuza Sekta ya Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

**166. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuimarisha mahusiano mazuri na Taasisi hizo, imefanya vikao vya ushirikiano na Wizara/Taasisi hizo kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano pamoja na kubadilishana uzoefu utakaosaidia kuimarisha na kuweka mikakati katika utoaji wa huduma na kukuza ushirikiano. Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi hizo kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na naziomba ziendeleze kutoa ushirikiano kwa maslahi mapana ya wananchi wetu.

## F. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO.

**167. Mheshimiwa Spika,** sekta binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa Anga, Baharini na Nchi kavu pamoja na huduma za Mawasiliano hapa Zanzibar.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine za kiuchumi na kijamii, kuchangia Pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kisera kwa sekta hizo ili iendelee kuimarisha huduma za Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

168. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi binafsi zinazotoa huduma za Usafirishaji na Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya na naziomba ziendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi.

## G. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

169. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, sasa naomba kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

170. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia sekta mbili kuu hapa Zanzibar ambazo ni Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji. Kwa kuzingatia Sekta hizo, Wizara ina Programu Kuu tatu (3) ambazo ni: - Programu ya Usafirishaji, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

## H. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

171. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika kuimarisha huduma za Mawasiliano na Usafirishaji hapa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imeweka vipaumbele katika kuimarisha miundombinu ya usafiri na huduma za mawasiliano kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo 2050 (Vision 2050), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 -2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar 2021- 2026, ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizozitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2020 pamoja na ahadi alizozitoa wakati akifanya ziara katika Mikoa na Wilaya kwa nyakati tofauti.

172. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuweka vipaumbele hivyo, Wizara imezingatia vipaumbele vikuu vya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwemo kuimarisha miundombinu ya usafiri wa Anga kwa kuanza maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja na kuendeleza ujenzi wa Uwanja wa Ndege Nungwi. Aidha, katika kuimarisha Sekta ya Usafiri wa Baharini, Wizara imepanga kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani (Intergrated Port) itakayojumuisha bandari za Mizigo, Chelezo, Mafuta na Gesi kwa kutafuta wawekezaji kuja kuwekeza katika Bandari hiyo katika maeneo tofauti yaliyoainshwa katika Mpango Mkuu (Master Plan) wa ujenzi wa bandari hiyo.

173. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imepanga kujenga na kuanza ujenzi wa barabara kuu nne (4) Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 125.6, kuendelea na ujenzi wa Barabara

za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 (**Kiambatanisho namba 3 kinahusika**) Unguja na Pemba pamoja na kuanza ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa kilomita 103.7 (**Kiambatanisho namba 4 kinahusika**). Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 200 za barabara zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 **(Kiambatanisho namba 5 kinahusika).**

## I. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**174. Mheshimiwa Spika,** programu kuu zilizoainishwa katika bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji. Maelezo ya programu hizo ni kama ifuatavyo:

### I.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.

**175. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 programu ya Usafirishaji ina programu ndogo moja (1) ambayo ni; Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

#### I.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

**176. Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Barabara

Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora za usafiri zilizo salama zinapatikana muda wote. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni:- uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa Barabara, Anga na Baharini, Utunzaji na Matengenezo ya barabara mbalimbali, Usimamizi wa Usafiri na Usalama Barabarani pamoja na matengenezo ya vyombo vya moto.

177. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 570,647,000,000 kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 6,640,000,000 ni ruzuku kwa kazi za kawaida na jumla ya TSH 564,007,000,000 zitatumika kwa kazi za maendeleo, ikiwa TSH 337,860,000,000 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 226,147,000,000 ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## I.2. PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).

178. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 programu hii ina programu ndogo moja (1) ambayo ni; Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

### I.2.1 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA

179. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasilino pamoja na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA

Zanzibar (ZICTIA) na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni usimamizi wa huduma za TEHAMA pamoja na usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.

180. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya TSH 3,456,640,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara kwa Taasisi zinazosimamia programu hii.

## I.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA.

181. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### I.3.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

182. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Programu hii ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi pamoja na kusimamia shughuli za kiutawala na utumishi katika Wizara.

183. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 2,618,597,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida na mishahara.

### I.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

184. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbalimbali za Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni utayarishaji na utekelezaji wa Bajeti pamoja na uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara.

185. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya TSH 1,030,728,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

### I.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

186. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika programu hii ndogo ni uratibu wa kazi za Wizara Pemba ikiwemo kusimamia shughuli za utawala na utumishi, mipango na bajeti, huduma za usafiri barabarani, huduma za TEHAMA pamoja na ujenzi, utunzaji na matengenezo ya barabara mbalimbali – Pemba.

187. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya TSH 1,040,954,000 kwa kazi za kawaida na mishahara.

## J. HITIMISHO

188. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na

kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza katika kipindi cha mwaka 2021/2022 na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zilizopangwa katika programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

189. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba hii ninayoiwasilisha kwenu, ni matokeo ya ushirikiano wa wahusika mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kuendeleza Sekta za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Saudi Fund na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo IMO na ICAO.

190. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, natoa shukurani zangu kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma za mawasiliano na usafirishaji hapa Zanzibar ikiwemo Kampuni za mawasiliano za Zantel, Tigo, Halotel, Airtel, Vodacom, TTCL na Zanlink. Kampuni za usafirishaji wa baharini ikiwemo African Shipping Corporation, Zanzibar Shipping Corporation, Kilimajaro Fast Ferries Marine Services Limited, Azam Marine, Zanzibar Fast Ferries na Ikraam Sealine Company.

Kwa upande wa usafiri wa anga tunazipongeza Kampuni za Air Tanzania, Assalam Air, Costal Travel, Auric Air, Unity Air, Pelican Air, Precission Air, Zan Air, Regional Air, Flight link, My Fly Aviation, Safari Air Link, Air Excel, Tropical Air, Fly Zanzibar na Kampuni za Kimataifa ikiwemo Ethiopian Airlines, Euro wings, Lufthansa Airline, Sky Up Airline, Turkish Airlines, Blue Panorama, Qatar Airlines, Fly Dubai, Kenya Airways, Global Airways, Oman Air, Uganda Air, Israil Airlines, KLM Airlines, 540 Aviation, Air Kenya na nyenginezo. Kwa upande wa Usafiri wa nchi kavu tunawapongeza na kuwashukuru wamiliki na watendaji wa vyombo vya usafiri wa nchi kavu ikiwemo Daladala, Magari ya Shamba, Bodaboda pamoja na Bajaji kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kufanikisha huduma za usafiri kwa wananchi.

**191. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi nikianza na Mheshimiwa Juma Makungu Juma Naibu Waziri ambae pia ni Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi katika Jimbo la Kijini, Ndugu Amour Hamil Bakari Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika na Taasisi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ushirikiano na juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru wale wote ambao wamechangia kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utayarishaji wa hotuba hii.

**192. Mheshimiwa Spika,** hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo langu la Donge kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokuwa mbali nao kutokana

na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee.

**193. Mheshimiwa Spika,** Ni matumaini yangu kwamba maelezo niliyotoa katika hotuba hii yanatosha katika kuliarifu Baraza lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi kilichopita na Mpango wa utekelezaji wa majukumu kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2022/2023. Hivyo ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wataichangia hotuba hii kwa kutukosoa pale tulipokosea, kutuweka sawa pale tulipoteleza na bila shaka kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara hii pale walipofanya vizuri.

## K. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023.

**194. Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutekeleza majukumu na malengo yake yaliyoainishwa katika Programu Kuu tatu (3) katika hotuba hii pamoja na utekelezaji wa Ilani Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **TSH 578,793,920,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**195. Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha hizo **TSH 14,786,920,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida, **TSH 337,860,000,000** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa maendeleo na **TSH 226,147,000,000** ni fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**196. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **TSH 7,028,974,000** kwa Wizara

ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Unguja na Pemba.

**197.** **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**198.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohamed (MBM)**
**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar**

## VIAMBATANISHO:

### Kiambatanisho Namba 1A: Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Julai 2021 - Machi 2022

| Aina ya chombo | Ukaguzi wa vyombo | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Unguja | Pemba | |
| Gari | 22,805 | 3,300 | 26,105 |
| Vyombo vya maringi mawili | 18,282 | 2,838 | 21,120 |
| **Jumla** | **41,087** | **6,138** | **47,225** |

### Kiambatanisho Namba 1B: Ruhusa za Njia na Usafirishaji Julai 2021- Machi 2022

| Sehemu ilipo-tolewa | Aina ya huduma iliyotolewa | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Daladala | Shamba | P/Hire | Taxi | Mizigo A | Mizigo C | W/fu nzi | W/kazi | Kuko-disha | Piki piki | Jumla |
| **Unguja** | **1025** | **950** | **2358** | **460** | **1566** | **2568** | **113** | **55** | **47** | **2048** | **11,190** |
| **Pemba** | 15 | 399 | 14 | 27 | 131 | 437 | 08 | 02 | 00 | 286 | 1319 |
| **Jumla** | **1,040** | **1,349** | **2,372** | **487** | **1,697** | **3,005** | **121** | **57** | **47** | **2,334** | **12,509** |

### Kiambatanisho Namba 1C: Utoaji wa Beji kwa Madereva na Matingo wa Gari za Abiria kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022.

| Aina ya Beji | Sehemu iliyotolewa | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Unguja | Pemba | |
| **Dereva** | 3,669 | 259 | 3,928 |
| **Utingo** | 3,267 | 380 | 3,647 |
| **Jumla** | **6,936** | **639** | **7,575** |

**Kiambatanisho Namba 2: Orodha ya Kazi za Matengenezo ya Barabara zilizopangwa Kutekelezwa kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 Kupitia Mfuko wa Barabara Zanzibar**

| Namba | Jina la Barabara | Kilomita |
|---|---|---|
| | **Unguja** | |
| **1.** | Ujenzi wa barabara ya Unguja Ukuu- Uzi - Ng'ambwa | 7 |
| **2.** | Ujenzi wa barabara ya Tumbatu | 9 |
| **3.** | Ujenzi wa barabara ya Garagara – Chemchem – Mtoni Kidatu | 3 |
| **4.** | Ujenzi wa barabara ya Kiboje- Uchukuni | 3.1 |
| **5.** | Ujenzi wa Daraja la Machui | |
| **6.** | Ujenzi wa Daraja la Mtopepo | |
| **7.** | Ujenzi wa Daraja la Pangatupu | |
| **Pemba** | | |
| 1. | Ujenzi wa barabara ya Kipapo - Mgelema - Wambaa | 9.3 |
| 2. | Ujenzi wa barabara ya Chanjamjawiri -Tundauwa | 11 |
| 3. | Ujenzi wa barabara ya Chanjaani - Pujini | 5 |
| 4. | Ujenzi wa barabara ya Mzingani – Wambaa | 9.7 |
| 5. | Ujenzi wa barabara ya Kenya – Chambani | 3.2 |
| 6. | Ujenzi wa barabara ya Mtambile – Kangani | 6.4 |
| 7. | Ujenzi wa barabara ya Mtambile – Kengeja | 9.4 |
| 8. | Ujenzi wa barabara ya Kijangwani - Birikau | 4.2 |
| 9. | Ujenzi wa Daraja la Vitongoji | |
| 10. | Ujenzi wa Daraja la Chamanangwe | |
| 11. | Ujenzi wa Daraja la Pondeani | |

**Kiambatanisho Namba 3: Orodha ya Barabara za Ndani zenye Urefu wa Kilomita 275.9 zinazotarajiwa Kujengwa kwa Kipindi cha Miaka Mitano**

| Namba | Jina la Barabara | Urefu (km) | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 1 | Mfurumatonga - Mbuyupopo | 3.3 | Kaskazini "A" |
| 2 | Bwekunduni - Soko la samaki | 2 | Kaskazini "A" |
| 3 | Mfurumatonga - Mlilile school - New Road | 2.4 | Kaskazini "A" |
| 4 | Mto wa Pwani - Fungurefu | 2 | Kaskazini "A" |
| 5 | Donge vijibweni-Chaani Masingini | 6 | Kaskazini "A" |
| 6 | Fukuchachani-Kidagoni Skuli - Kidoti | 6.5 | Kaskazini "A" |
| | **Jumla Kaskazini "A"** | **22.2** | |
| 7 | Mahonda – Zingwezingwe - M/pwani | 7.6 | Kaskazini "B" |
| 8 | Mahonda – Pangatupu - Bumbwini | 8 | Kaskazini "B" |
| 9 | Muanda - Msikitini | 0.6 | Kaskazini "B" |
| 10 | Donge mbiji - Chechele | 2 | Kaskazini "B" |
| 11 | Bumbwini Skuli - Kiongwe | 4.3 | Kaskazini "B" |
| 12 | Upenja – Kibumbwi Skuli | 1.5 | Kaskazini "B" |
| | **Jumla Kaskazini "B"** | **24** | |
| 13 | Jangombe School - Soko la mboga Mpendae | 2.2 | Mjini |
| 14 | Shaurimoyo - Mboriborini - Sebleni+ Kwamtipura spur | 2 | Mjini |
| 15 | Mwembe Makumbi - Mtopepo School | 1.8 | Mjini |
| 16 | Magereza (Tumbaku) - Maktaba Junction | 0.4 | Mjini |
| 17 | Kisiwandui - CRDB - Kikwajuni CCM | 0.4 | Mjini |
| | **Jumla Mjini** | **6.8** | |
| 18 | Kama msikitini - Kama KMKM | 3 | Magharibi "A" |
| 19 | Bumbwisudi - Kizimbani | 3.3 | Magharibi "A" |
| 20 | Mwakaje – Mwachealale - Bumbwisudi | 4.9 | Magharibi "A" |
| 21 | Masingini - Kijichi | 8 | Magharibi "A" |
| 22 | Mtoni Kidatu - Miembe 7 (Makufuli) | 2.3 | Magharibi "A" |

| Namba | Jina la Barabara | Urefu (km) | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 23 | Kibweni KMKM - Mwanyanya Msikitini - KVZ | 4.3 | Magharibi "A" |
| 24 | Mwera Police - Kibondemzungu | 6.1 | Magharibi "A" |
| | **Jumla Magharibi "A"** | **31.9** | |
| 25 | Dimani market - Dimani beach | 1.8 | Magharibi "B" |
| 26 | Kombeni - Nyamanzi | 1 | Magharibi "B" |
| 27 | Jumbi Sokoni – Kibondeni School - Hospital | 4.4 | Magharibi "B" |
| 28 | Tomondo Magereza - Kwarara | 2.7 | Magharibi "B" |
| 29 | Tomodo – Changu - Viwanja vya Magereza | 0.75 | Magharibi "B" |
| 30 | Msikiti wa Othman Maalim - Kwerekwe Sokoni | 0.7 | Magharibi "B" |
| | **Jumla Magharibi "B"** | **16.35** | |
| 31 | Mchangani - Dongongwe | 4.3 | Kati |
| 32 | Kidimni - Ubago | 4.3 | Kati |
| 33 | Jumbi - IPA - Tunguu (Ringroad) | 5 | Kati |
| 34 | Tunguu - Ndijani Mseweni - Mkwajungoma | 7.8 | Kati |
| 35 | Mgenihaji - Kwambani | 2.4 | Kati |
| | **Jumla Kati** | **22.9** | |
| 36 | Jambiani Kibigija - Jambiani Mfumbwi | 5 | Kusini |
| 37 | Muungoni School - Pwani Duta | 2.6 | Kusini |
| 38 | Bwejuu - Viamboni Kwa lila | 1.9 | Kusini |
| 39 | Kajengwa – Koba – Kinandi - Mnarani | 6 | Kusini |
| 40 | Mtandao - Chiabonde | 1.3 | Kusini |
| | **Jumla Kusini** | **16.8** | |
| | **Jumla Kuu - Unguja** | **140.95** | |
| 41 | Ukutini - Mtangani Bandari | 4 | Mkoani |
| 42 | Mtambile - Mwakunguu | 4.7 | Mkoani |
| 43 | Jambang'ome Jct - Jambangome | 2.4 | Mkoani |
| 44 | Mgagadu - Kwautao | 5.6 | Mkoani |

| Namba | Jina la Barabara | Urefu (km) | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 45 | Kengeja - Shamiani + Kiimbini spur | 4.4 | Mkoani |
| 46 | Mbuguani - Tironi | 3 | Mkoani |
| | **Jumla Mkoani** | **24.1** | |
| 47 | Wesha - Mkumbuu | 10 | Chake |
| 48 | Wawi Mesi - Mzambaraumboko | 6.4 | Chake |
| 49 | Mkoroshoni(zbc) – Ndugukitu - Machomane | 2 | Chake |
| 50 | Mchangakwale -Kichuani port | 2.7 | Chake |
| 51 | Chanjamjawiri - Pujini (Matale) | 4.3 | Chake |
| 52 | Barawa - Mleteni | 2 | Chake |
| 53 | Mavapacha - Mabaoni | 2.1 | Chake |
| | **Jumla Chake Chake** | **29.5** | |
| 54 | Mapofu - Tumbe Kojifa - Bandarini | 12.7 | Micheweni |
| 55 | Finya - Kicha | 8.6 | Micheweni |
| 56 | Micheweni – Kiuyu - Maziwa Ngombe | 7.5 | Micheweni |
| 57 | Konde - Msuka | 4.1 | Micheweni |
| 58 | Konde - Makangale | 12 | Micheweni |
| 59 | Micheweni - Shumba mjini - Bandarini | 2.5 | Micheweni |
| | **Jumla Micheweni** | **47.4** | |
| 60 | Makongeni - Kinazini | 3.2 | Wete |
| 61 | Uondwe - Nyali | 1.5 | Wete |
| 62 | Bwagamoyo - Kele | 6.5 | Wete |
| 63 | Gando - Chokaani | 2.1 | Wete |
| 64 | Gando - Chaoni | 1.5 | Wete |
| 65 | Kizimbani - Uzunguni | 1 | Wete |
| 66 | Mkarafuummoja - Jumapili | 5.15 | Wete |
| 67 | Kiungoni - Tovuniu | 1.5 | Wete |
| 68 | Pembeni - Pandani | 3.3 | Wete |
| 69 | Mzambarau takao - Mchangamdogo | 6 | Wete |

| Namba | Jina la Barabara | Urefu (km) | Wilaya |
|---|---|---|---|
| 70 | Penjewani - Mjini Kiuyu | 2.2 | Wete |
| | **Jumla Wete** | **33.95** | |
| | **Jumla Kuu - Pemba** | **134.95** | |
| | **Jumla Kuu - Unguja na Pemba** | **275.9** | |

**Kiambatanisho Namba 4: Orodha ya Barabara za Mjini zenye Urefu wa Kilomita 103.7**

| Na | Jina la Barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 1 | Abeid Amani Karume International Airport - Kiinua Miguu (Magereza) | 5.5 |
| 2 | K/Samaki Junction - Amani - Mtoni Junction (Mkapa Road) | 8.5 |
| 3 | Kariakoo - Magomeni - M/Kwerekwe | 3.7 |
| 4 | Kinazini Junction (BOT) - Mtoni Junction | 3.0 |
| 5 | Amani Roundabout – Mikunguni – Bizired | 2.5 |
| 6 | Mazizini Junction - ZRB - Mombasa Roundabout | 0.6 |
| 7 | Ng'ambo Police Station - Mfereji wa Wima | 0.3 |
| 8 | Mazizini Police Station - Chukwani Jeshini Road | 4.6 |
| 9 | Mazizini Vitambulisho - Zanzibar Beach Resort - Fish Market na Associated Roads | 3.2 |
| 10 | Mazizini (Vp2 Residence House) - Migombani (Ali Mzee) na Associated Access Roads | 0.9 |
| 11 | Miembeni Roundabout - Michenzani Block Number 1 na 9 | 0.5 |
| 12 | Miembeni Roundabout - Bomani - K/Chekundu Mental Hospital | 1.2 |
| 13 | Saateni JKU - Kwaali Msha | 1.3 |

| Na | Jina la Barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 14 | Jang'ombe Junction – Matarumbeta | 0.6 |
| 15 | Gulion Gapco - Makadara - Kwa Abasi Hussen | 0.6 |
| 16 | Kijagwani Posta - Muembeladu Hospital - Miti Ulaya | 0.7 |
| 17 | Mtendeni - Michenzani Road and Associated Streets | 0.7 |
| 18 | Michenzani Block Number 10&5 - Gongoni - Kisiwa Ndui - Msikiti Mabati - Hailesalas and Associated Street Roads | 1.3 |
| 20 | Benbella- Kikwajuni/ Maisra/Kikwajuni-Mau Stadium and Associated Streets | 1.2 |
| 22 | Mtoni Deport - ZECCO Power Station - Mtoni Kidatu | 0.7 |
| 23 | Mwebe Makubi - Basra - Karakana Mtapepo School | 1.6 |
| 24 | Rahaleo ZBC - Bizired na Associated Street Roads | 3.1 |
| 25 | Mpendae Planned Area | 13.3 |
| 26 | Chukwani Mwisho – Buyu | 3.5 |
| 27 | Kilimani Bar - Jang'ombe | 0.5 |
| 28 | Kwakira - Kituo Kipya Cha Uwanja Wa Ndege - Baraza La Uwakilishi | 1.6 |
| 29 | Mbweni Afya - Madina - Mbweni Matrekta | 2.4 |
| 30 | Zssf Mbweni Estates (Formerly Bima Quarters) - Mbweni Ruins Plus Mbweni - BOT Quarter - Kiembesamaki Main Road and Associate | 4.8 |
| 32 | River Tiba - Chukwani School - Chukwani Tuta and Associated Access Roads | 5.0 |
| 33 | Daraja Bovu - Faraja Skuli - Mboriborini - Shauri Moyo Skuli -Saateni | 2.1 |

| Na | Jina la Barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 36 | Makadara - Mfereji Wa Wima | 0.5 |
| 38 | Magazeti Press – Mkele | 0.4 |
| 39 | Msikiti Shurba – Mshelishelini – Matarumbeta | 0.6 |
| 40 | Muembenjugu - Mikunguni & Begamoja - Muungano and Associated Roads | 1.3 |
| 41 | Mnara Mbao - Migombani Garden | 0.3 |
| 42 | Kwakira – Kwajastuma | 1.0 |
| 43 | Mombasa Planned Area | 5.9 |
| 44 | Msumbubiji Kinyan'gunya - Mwanakwerekwe and Associated Roads | 5.4 |
| 45 | Mwanakwerekwe Gapco - Kwerekwe Skuli – Kanisani - Kwamchina and Associated Road | 6.0 |
| 46 | Barabara ya Malindi - Maruhubi | 3.2 |
| 47 | Construction of Fly Over or Widening of Roundabout (Amani and Mwanakwerekwe Roundabout) | |
| | **Jumla Kuu** | **103.7** |

**Kiambatanisho Namba 5: Orodha ya Barabara zenye Urefu wa Kilomita 200**

| Namba | Barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 1 | Kinazini - Mtoni – Bububu | 10.20 |
| 2 | Welezo - Amani - Ng'ambu | 2.90 |
| 3 | Kwanyanya - Mbuzini – Mkanyageni | 3.80 |
| 4 | Bububu Polisi – Mndo | 3.00 |
| 5 | Kizimbani – Kiboje | 7.20 |
| 6 | Kichwele – Pangeni | 4.80 |
| 7 | Mkwajuni – Kijini | 9.40 |
| 8 | Jozani - Charawe - Ukongoroni – Bwejuu | 23.30 |
| 9 | Umbuji – Uroa | 6.90 |
| 10 | Muyuni (Matemwe)- Nungwi | 13.00 |
| 11 | Mshelishelini – Pwani Mchangani | 7.50 |
| 12 | Kinyasini – Kiwengwa | 10.00 |
| 13 | Mahonda – Donge – Mkokotoni | 13.00 |
| 14 | Kizimkazi – Makunduchi | 13.00 |
| 15 | Kitogani – Paje | 11.00 |
| 16 | Dunga – Chwaka – Pongwe | 30.00 |
| | Jumla Unguja (km) | 169.00 |
| 17 | Chwale – Kilindini – Konde Sokoni | 25.00 |

| Namba | Barabara | Urefu (km) |
|---|---|---|
| 18 | Kilindini – Micheweni | 6.00 |
| | **Jumla Pemba (km)** | **31.00** |
| | **Jumla Kuu (km)** | **200.00** |

**Kiambatanisho Namba 6: Orodha ya Miradi inayotarajiwa Kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Namba | Jina la Mradi | Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Mchango wa Washirika wa Maendeleo | Jumla |
| 1. | Ujenzi wa Barabara za ndani Unguja na Pemba km 275.9 | 30,000,000,000 | - | 30,000,000,000 |
| 2. | Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja km 100 | 135,600,000,000 | - | 135,600,000,000 |
| 3. | Ujenzi wa Barabara Kuu 4 Zanzibar | 37,947,000,000 | 211,760,000,000 | 249,707,000,000 |
| 4. | Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 8,000,000,000 | 126,100,000,000 | 134,100,000,000 |
| 5. | Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi | 6,600,000,000 | - | 6,600,000,000 |
| 6. | Ujenzi wa Bandari Jumuishi-Mangapwani | 8,000,000,000 | - | 8,000,000,000 |
| | **Jumla** | **226,147,000,000** | **337,860,000,000** | **564,007,000,000** |

**Kiambatanisho Namba 7A: Orodha ya Taasisi zilizounganishwa na Mkonga wa Mawasiliano kwa Kipindi cha Julai, 2021 – Machi, 2022**

| Namba | Unguja |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) |
| 2. | Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Mjini Magharibi |
| 3. | Zanzibar Food and Drug Agency (ZFDA) |
| 4. | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana |
| 5. | Wakala wa Serikali Mtandao |
| 6. | Haiba TV |
| 7. | Nyumba ya Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar |
| 8. | Kwarara Media Education Centre (KMEC) |
| 9. | Alfa care |
| 10. | Nyumba ya Mheshimiwa Ali Mohamed Shein Rais Mstaafu (Kibele) |
| 11. | Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar (IPA) |
| 12. | Nyumba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 13. | Mahakama Kuu Zanzibar |
| 14. | Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari kuu (DEEP Sea) |
| 15. | China Medical |
| 16. | Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) |
| 17. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda |
| 18. | Wizara ya Uchumi wa Buluu |
| 19. | Wizara ya Maji na Nishati |
| 20. | Zanzibar Shipping Line LTD |
| 21. | Nyumba ya Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi |

| | |
|---|---|
| | Zanzibar |
| 22. | Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA - Vuga) |
| 23. | Uwanja wa Mpira wa Amani (Amani Stadium) |
| 24. | Halmashauri Wilaya ya Kusini Unguja |
| 25. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - Kitogani |
| 26. | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja |
| 27. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - Kinduni |
| 28. | Makao Makuu ya KMKM - Kibweni |
| 29. | Kituo cha Kurushia Matangazo kwa Njia ya Redio (WEMA - Masingini) |
| 30. | Chuo Kikuu cha Zanzibar (Suza - Kizimbani) |
| 31. | Ofisi ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja |
| 32. | Nyumba ya Mheshimiwa Ali Mohd Shein Rais Mstaafu –Mazizini |
| **Pemba** | |
| 1. | Zanzibar Bureau of Standard (ZBS Wete) |
| 2. | Baraza la Mji – Wete |
| 3. | Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Micheweni |
| 4. | Ikulu Chake Chake |
| 5. | Mamlaka ya Maji Zanzibar Chake Chake |
| 6. | Zanzibar Bureau of Standard (ZBS - Chake Chake) |
| 7. | Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) - Mkoroshoni |
| 8. | Zanzibar Bureau of Standard (ZBS - Mkoani) |
| 9. | Ikulu – Mkoani |

**Kiambatanisho Namba 7B: Taasisi zilizounganishwa na Data Centre kwa Kipindi cha Julai, 2021 – Machi, 2022**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar |
| 2. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar |
| 3. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar |
| 4. | Shirika la Meli Zanzibar |
| 5. | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Zanzibar |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi A |
| 7. | Wizara ya Afya |

**Kiambatanisho Namba 8: Orodha ya Minara ya Mawasiliano inayoendelea Kujengwa katika Maeneo Mbalimbali Unguja na Pemba**

| Namba | Mkoa | Wilaya | Wadi | Vijiji | Idadi ya Vijiji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kask Pemba | Micheweni | Konde | Msuka Magharibi, Msuka Mashariki, Msuka | 3 |
| 2 | Kask Pemba | Micheweni | Tumbe | Mihogoni, Wingwi Mapofu, Shumba Viamboni | 3 |
| 3 | Kask Pemba | Wete | Kiungani | Mlindo | 1 |
| 4 | Kask Pemba | Wete | Mchangamdogo | Mchangamdogo | 1 |
| 5 | Kask Pemba | Wete | Ukunjwi/ Fundo | Fundo | 1 |
| 6 | Kask Pemba | Wete | Ukunjwi/ Fundo | Ukunjwi | 1 |
| 7 | Kask Unguja | Kask A | Chaani Kubwa | Chaani Kubwa, Bandamaji, kikobweni | 3 |
| 8 | Kask Unguja | Kask A | Fukuchani | Fukuchani, kigongoni | 2 |
| 9 | Kask Unguja | Kask A | Kandwi | Kandwi | 1 |
| 10 | Kask Unguja | Kask A | Kigunda | Kigunda, Tazari, kilimani Tazari | 3 |

| Namba | Mkoa | Wilaya | Wadi | Vijiji | Idadi ya Vijiji |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Kask Unguja | Kask A | Matemwe | Matemwe, Kijini Matemwe | 2 |
| 12 | Kask Unguja | Kask A | Mbuyutende | Mbuyutende, Kijini | 2 |
| 13 | Kask Unguja | Kask A | Mkokotoni | Mkokotoni, Mto wa Pwani | 2 |
| 15 | Kask Unguja | Kask A | Potoa | Potowa | 1 |
| 16 | Kask Unguja | Kask B | Donge Mtambile | Donge Mtambile, donge Vijibweni, Njia ya Mtoni | 3 |
| 17 | Kask Unguja | Kask B | Mangapwani | Mangapwani, Fujoni, Zingwezingwe | 3 |
| 18 | Kask Unguja | Kask B | Mgambo | Mgambo, Kinduni | 2 |
| 19 | Kask Unguja | Kask B | Pangeni | Pangeni, Kilombero | 2 |
| 20 | Kus Pemba | Chakechake | Kilindi | Kilindi | 1 |
| 21 | Kus Pemba | Chakechake | Matale | Mfikiwa | 1 |
| 22 | Kus Pemba | Chakechake | Ndagoni | Wesha-Birikau, Wesha School, Michungwani | 3 |
| 23 | Kus Pemba | Chakechake | Ngambwa | Vikunguni; Shigiwana | 2 |
| 24 | Kus Pemba | Chakechake | Uwandani | Uwandani/Kangagani | 1 |
| 25 | Kus Pemba | Mkoani | Kengeja | Kimbini, Shamiani | 2 |
| 26 | Kus Pemba | Wete | Mgagadu | Mgagadu | 1 |
| 27 | Kus Unguja | Kati | Bambi | Mchangani Shamba, Kijibwemtu | 2 |
| 28 | Kus Unguja | Kati | Bambi | Bambi, Umbuji | 2 |
| 29 | Kus Unguja | Kati | Bungi | Tindini, Uzi | 2 |
| 30 | Kus Unguja | Kati | Bungi | Ng'ambwa | 1 |
| 31 | Kus Unguja | Kati | Kiboje | Mwembeshauri, Uzini, Kiboje Mkwajuni, Mgeni Haji | 4 |
| 32 | Kus Unguja | Kati | Tunguu | Binguni | 2 |
| 33 | Kus Unguja | Kati | Ubago | Dunga Bweni, Dunga Kiembeni | 2 |
| 34 | Kus Unguja | Kati | Ubago | Ubago, Kidimni | 2 |
| 35 | Kus Unguja | Kus | Jambiani | Muungoni | 1 |
| 36 | Kus Unguja | Kus | Muyuni | Muyuni 'A', B, C, Kibuteni, Mtende | 5 |
| 37 | Mjini West | Magh A | Kianga | Mkangeni | 1 |
| 38 | Mjini Magh | Magh B | Chukwani | Shakani | 1 |
| 39 | Mjini Magh | Magh B | Fuoni Kibondeni | Fuoni Chunga | 1 |

| Namba | Mkoa | Wilaya | Wadi | Vijiji | Idadi ya Vijiji |
|---|---|---|---|---|---|
| 40 | Mjini Magh | Magh A | Bububu | Mbuzini | 1 |
| 41 | Mjini Magh | Magh A | Dole | Chemchem, Kizimbani | 2 |
| 42 | Mjini Magh | Magh A | Mfenesini | Mwakaje, Bumbwisudi | 2 |
| | **Jumla** | | | | **80** |

**Kiambatanisho Namba 9A: Wafanyakazi waliopata Mafunzo ya Muda Mrefu kwa Kipindi cha Mwaka 2021/2022**

| Idara/Taasisi | Phd | | Shahada ya Uzamili | | Shahada ya Kwanza | | Stashahada ya Juu | | Diploma | | Cheti | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | Ke | Me | |
| Uendeshaji na Utumishi | - | - | 1 | - | 1 | 2 | - | - | - | - | - | - | 4 |
| Mipango, Sera na Utafiti | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mawasiliano | - | 1 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Ofisi kuu Pemba | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Jumla Kuu** | **-** | **1** | **1** | **-** | **1** | **2** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **5** |

**Kiambatanisho Namba 9B: Wafanyakazi waliopata Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Kipindi cha Mwaka wa fedha 2021/2022**

| Idara/ Taasisi | W/Ke | W/Me | Jumla |
|---|---|---|---|
| Uendeshaji na Utumishi | 6 | 5 | **11** |
| Idara ya Mawasiliano | 3 | 1 | **4** |
| Mipango, Sera na Utafiti | 4 | 7 | **11** |
| Ofisi Kuu - Pemba | - | - | **-** |
| **Jumla Kuu** | **13** | **13** | **26** |

**Kiambatanisho Namba 10: Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo zilizopatikana kwa kila Programu kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022**

| Namba | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio 2021/2022 | Matumizi Halisi Julai 2021 hadi Machi 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **1** | **Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafirishaji** | | | |
| 1.1 | Usimamizi wa Usafirishaji | 3,266,100,000 | 1,519,994,796 | 46.5 |
| 1.2 | Miundombinu ya Usafirishaji | 136,699,766,000 | 38,292,178,529 | 28.01 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **139,965,866,000** | **39,812,173,325** | **28.4** |
| **2** | **Programu ya Miundombinu na Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)** | | | |
| 2.1 | Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA | 2,210,500,000 | 1,686,507,779 | 76.3 |
| 2.2 | Usimamizi wa Huduma za TEHAMA | 1,304,275,000 | 326,048,397 | 25 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **3,514,775,000** | **2,012,556,176** | **57.2** |
| **3** | **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | | |
| 3.1 | Utawala na Uendeshaji | 2,310,366,000 | 1,074,150,058 | 47 |
| 3.2 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 801,336,000 | 336,805,929 | 42 |
| 3.3 | Uratibu wa Shughuli za Wizara – Pemba | 1,003,222,000 | 387,179,925 | 38.6 |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **4,114,924,000** | **1,798,135,912** | **43.7** |
| | **Jumla Kuu ya Programu Kuu za Wizara** | **147,595,566,000** | **43,622,865,413** | **29.5** |

**Kiambatanisho Namba 11: Mapato yaliyokusanywa kwa Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022**

| Namba | Taasisi /Idara. | Makadirio Julai 2021 hadi Machi 2022 | Fedha Zilizokusanywa Julai 2021 - Machi 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ofisi Kuu Pemba | 650,119,250 | 304,504,000 | 46.8 |
| 2. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | 1,926,335,250 | 2,179,094,302 | 113 |
| 3. | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA | 1,758,602,250 | 2,291,981,194 | 130 |
| | **Jumla** | **4,335,056,750** | **4,775,579,496** | **110** |

**Kiambatanisho Namba 12A: Idadi ya Ndege zilizohudumiwa kwa Kipindi cha Julai 2021 - Machi 2022**

| Namba | Aina ya ndege | Idadi ya ndege | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | |
| 1. | Ndege zenye ratiba (schedule) | 25,679 | 3,570 | **29,249** |
| 2. | Ndege zisizo na ratiba (charter) | 5,630 | 294 | **5,924** |
| 3. | Mizigo (cargo) | 22 | - | **22** |
| 4. | Binafsi (private) | 55 | - | **55** |
| 5. | Kijeshi (military) | 38 | 6 | **44** |
| 6. | Nyenginezo | 1,226 | 34 | **1,260** |
| | **Jumla** | **32,650** | **3,904** | **36,554** |

**Kiambatanisho Namba 12B: Idadi ya Abiria waliohudumiwa katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022**

| Uwanja | Idadi ya Abiria 2021/2022 | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | wa Kigeni | wa Ndani | |
| AAKIA | 545,055 | 362,782 | **907,837** |
| Pemba Airport | 12 | 66,126 | **66,138** |
| **Jumla** | **545,067** | **428,908** | **973,975** |

**Kiambatanisho namba 12C: Kampuni za Ndege zilizotumia Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kwa Mwaka 2021/2022**

| Namba | Jina la Kampuni | Vituo | Nchi inayotoka |
|---|---|---|---|
| **Kampuni za Ndani** | | | |
| 1 | Air Tanzania | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 2 | Coastal Travel | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 3 | Precision Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 4 | Air Excel | Dar, Zanzibar | Tanzania |
| 5 | Auric Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 6 | Zan Air | Dar, Zanzibar | Tanzania |
| 7 | Unity Air | Pemba, Zanzibar | Tanzania |
| 8 | Assalam Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 9 | Flight Link | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 10 | Pelican Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 11 | Regional Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 12 | My Fly Aviation | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 13 | Safari Plus | Dar, Zanzibar | Tanzania |
| 14 | Safari Air Link | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 15 | Twin Wing | Dar, Zanzibar | Tanzania |
| 16 | Tanzania Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 17 | Tropical Air | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 18 | Jambo Aviation | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 19 | Fly Zanzibar | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| 20 | ZRP | Dar, Zanzibar | Tanzania |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21 | Zantas Air | Dar, Zanzibar | Tanzania |
| 22 | Moss Wood | Dar, Zanzibar, Pemba | Tanzania |
| **Kampuni za Kimataifa** | | | |
| 1. | Ethiopian Airlines | Addis – Ababa, Zanzibar | Ethiopia |
| 2. | 540 Aviation | Mombasa, Zanzibar, Nairobi | Kenya |
| 3. | Fly Dubai | Dubai, Zanzibar | Dubai |
| 4. | Global Airways | Johannesburg, Zanzibar | South Africa |
| 5. | Kenya Air | Nairobi, Zanzibar | Kenya |
| 6. | Euro wings | Frankfurt, Zanzibar | Germany |
| 7. | Oman Air | Muscat, Zanzibar | Oman |
| 8. | Israel Air | Telaviv, Zanzibar | Israel |
| 9. | Lufthansa Airline | Frankfurt, Zanzibar | Germany |
| 10. | Flying Doctor | Nairobi, Zanzibar | Kenya |
| 11. | Astral Aviation | Kenya, Zanzibar | Kenya |
| 12. | Azzur Air | Moscow, Zanzibar | Russia |
| 13. | Sky Up Airline | Ukraine, Zanzibar | Ukraine |
| 14. | Turkish Airline | Istanbul, Zanzibar | Turkey |
| 15. | Qatar | Doha | Qatar |
| 16. | Blue Panorama | Milan, Zanzibar | Italy |
| 17. | Air Kenya | Nairobi, Zanzibar | Kenya |
| 18. | Polish Air | Poland, Zanzibar | Poland |
| 19. | UT Air Aviation | Moscow, Zanzibar | Russia |
| 20. | Uganda Air | Kampala, Dar, Zanzibar | Uganda |
| 21. | KLM Airlines | Belgium, Zanzibar | Belgium |
| 22. | Enter Air | Poland, Zanzibar | Poland |
| 23. | Edelweiss | Swiss | Switzerland |
| 24. | Air France | Paris, Zanzibar | Paris |
| 25. | Etihad | Abu Dhabi, Zanzibar | Abu Dhabi |

**Kiambatanisho Namba 13A: Huduma za Meli**

| Namba | Aina ya Meli | Kipindi | | Ongezeko/ Punguzo (%) |
|---|---|---|---|---|
| | | Julai 2020 – Machi, 2021 | Julai 2021 – Machi 2022 | |
| 1. | Meli za Nje | 100 | 95 | (5) |
| 2. | Uzito wa Meli (GRT) | 1,097,821 | 1,145,671 | 104 |
| 3. | Meli za Ndani | 3,362 | 3,632 | 8 |
| 4. | Majahazi | 5,201 | 8,181 | 59 |

**Kiambatanisho Namba 13B: Huduma za Mizigo**

| Namba | Aina ya Mizigo | Muda wa Utekelezaji | | Ongezeko/ Punguzo (%) |
|---|---|---|---|---|
| | | Julai 2020 – Machi, 2021 | Julai 2021 Machi, 2022 | |
| 1. | Mzigo Mchanganyiko | 587,215 | 719,630 | 23 |
| 2. | Makontena<br>TEUs | 36,437<br>48,755 | 37,743<br>50,734 | 4<br>4 |
| 3. | Mzigo wa Majahazi | 75,172 | 209,927 | 179 |